


UKURASA 11

**NHIF** yawatoa hofu wanachama huduma kadi zake

UKURASA 8

**WAZAZI** wasiopeleka watoto wao shuleni kukiona cha moto

UKURASA 10



**UTAWALA** Hamas wasambaratishwa Gaza Kaskazini

UKURASA 19


# Nipashe

Jumatatu Januari 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581549

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa, Dk. Said Mohamed.

## MATOKEO LA IV, KIDATO CHA II

# Udanganyifu mfupa mgumu

**206** wafutiwa matokeo, 17 waandika matusi; Hisabati, Fizikia bado kizungumkuti, 212,000 'wakacha' mtihani...

*Endelea ukurasa 2*




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Mwekezaji wa Mradi wa Hoteli ya Crown and Resort Zanzibar, Gavin Faull, wakati wa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa hoteli hiyo huko Mazizini, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

### ASKOFU DK. SHOO: SERIKALI IHESHIMU MAONI YA WADAU SHERIA UCHAGUZI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, ametoa wito kwa serikali kuyaheshimu na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na wadau wakiwamo viongozi wa dini kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi...

UKURASA WA 14

### WACHEZAJI 8 WAZAWA MBIONI KUHAMA KATIKA DIRISHA HILI

KWA miaka ya hivi karibuni mashabiki wa soka nchini wamekuwa wakifurahishwa au kuridhishwa zaidi na usajili wa wachezaji kutoka nje ya nchi. Pamoja na hayo kuna baadhi...

## MAZUNGUMZO NA RUBANI

# Kilichojificha ndege kukosa kiti Na. 13

**ATAJA** kosa la kumpa kesi ya kujibu mahakamani, wajawazito kuzuiwa... *Endelea ukurasa* 4


**MICHEZO** GAMONDI AWAANDALIA MFUMO WAPAKI BASI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

## MATOKEO LA IV, KIDATO CHA II

# Udanganyifu mfupa mgumu

**Na Romana Mallya**



BARAZA la Mitihani la Taifa (NECTA) limetangaza matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili Mwaka 2023, huku wanafunzi 206 wakifutiwa matokeo yote kutokana na kufanya udanganyifu na wengine 17 kwa kuandika lugha za matusi.

Matokeo hayo pia yameonesha masomo ya Fizikia, Kemia, Kilimo na Hisabati yana ufaulu ulio chini ya wastani kati ya asilimia 19.06 hadi asilimia 39.24.

Vilevile, imebainishwa kuwa wanafunzi 211,997 wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili hawakufanya upimaji huo huku idadi kubwa ikiwa ni kwa wavulana.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, akitangaza matokeo hayo jana mkoani Dar es Salaam kwa waandishi wa habari, alisema baraza limefuta matokeo yote ya wanafunzi 178 waliofanya udanganyifu Darasa la Nne na watatu kati yao walioandika matusi kwenye skripti zao.

Dk. Mohamed alisema katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili, wanafunzi 28 waliofanya udanganyifu na 14 waliandika matusi kwenye skripti zao nao wamefutiwa matokeo.

"Matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5(2)(j) cha Sheria ya Baraza, Sura ya 107 kikisomwa pamoja na Kifungu cha 30(2)(b) cha sheria (2016).

"Matusi hayo ni jambo la kimaadili, utashangaa katika upimaji huu wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili, kuna somo la Maadili, lipo somo linaitwa somo la Maadili, ndani ya somo hili unaona kuna mtahiniwa ameandika matusi.

"Tumetahini watoto milioni 1.3, lakini unaona walioandika matusi ni watatu (Darasa la Nne) hata ukiweka hii asilimia ni asilimia 0.000 kwa hivyo, hawakosekani hao katika jamii," alisema.

Kuhusu hatua wanazochukua, Dk. Mohamed alisema wanaziandikia mamlaka zao za nidhamu kuwachukulia hatua, lakini kuwapa malezi mazuri na kufuatilia mienendo yao.

Alisema kuwa baada ya matokeo hayo, shule pamoja na wakuu wa shule wanakwenda kutaarifiwa rasmi vyote vilivyojiri katika mtihani huo.

**HALI ILIVYO**

Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi 1,693,444 walisajiliwa kufanya upimaji huo wakiwamo wasichana 864,482 sawa na asilimia 52.05 na wavulana 828,962 sawa na asilimia 48.95.

Alibainisha kuwa kati ya wanafunzi waliosajiliwa, wanafunzi 1,545,607 walifanya upimaji, wakiwamo wasichana 803,647 sawa na asilimia 92.96 na wavulana 741,960 sawa na asilimia 89.5.

"Wanafunzi 147,837 sawa na asilimia 8.73 hawakufanya upimaji. Kati yao, wasichana ni 60,835 sawa na asilimia 7.04 na wavulana ni 87,002 sawa na asilimia 10.50," alisema.

Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi 759,799 walisajiliwa kufanya upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili wakiwamo wasichana 405,878 sawa na asilimia 53.42 na wavulana ni 353,921 sawa na asilimia 46.58.

Alisema kati ya wanafunzi waliosajiliwa, 695,639 walifanya upimaji huo, wakiwamo wasichana 376,927 sawa na asilimia 92.87 na wavulana 318,712 sawa na asilimia 90.05.

"Wanafunzi 64,160 sawa na asilimia 8.44 hawakufanya upimaji, kati yao wasichana ni 28,951 sawa na asilimia 7.13 na wavulana ni 35,209 sawa na asilimia 9.95," alisema.

**MATOKEO YA UPIMAJI**

Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi 1,287,934 kati ya 1,545,330 wenye matokeo sawa na asilimia 83.34 wamefaulu kwa kupata madaraja A, B, C, D.

Alisema mwaka 2022 wanafunzi waliofaulu walikuwa 1,320,700 sawa na asilimia 82.95. Hivyo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 0.39 wa wanafunzi wanaoendelea na darasa la tano kulinganishwa na mwaka 2022.

Alisema kati ya waliofaulu kuendelea na darasa la tano, wasichana ni 681,259 sawa na asilimia 84.79 na wavulana 606,675 sawa na asilimia 81.78. Takwimu zinaonesha wasichana wamefaulu vizuri kuliko wavulana.

Mtendaji huyo alisema ufaulu wa shule katika makundi ya umahiri, unaonesha kuwa kati ya shule zote 19,264 zenye matokeo ya upimaji darasa la nne mwaka 2023, shule 18,939 sawa na asilimia 98.31 zimepata wastani wa daraja A-D kulinganishwa na shule 18,319 sawa na asilimia 98.27 zilizopata wastani wa madaraja hayo mwaka 2022.

Alisema kumekuwa na ongezeko la asilimia 0.04 ya shule zilizopata wastani wa daraja la A-D kulinganishwa na mwaka 2022.

Pia alisema ufaulu wa somo la Kiswahili ni wa asilimia 84.15, ukipanda kwa asilimia 0.96 na ufaulu wa somo la Kiingereza ni wa asilimia 72.54, ukipanda kwa asilimia 0.82 kulinganishwa na mwaka 2022.

Katika masomo ya lugha, Dk. Mohamed alisema wasichana wana ufaulu mkubwa zaidi kuliko wavulana ambapo somo la Kiswahili wasichana wamefaulu zaidi kuliko wavulana kwa asilimia 3.67 na somo la Kiingereza wasichana wamefaulu zaidi kuliko wavulana kwa asilimia 5.2.

Alisema ufaulu wa somo la Maarifa ya Jamii na Uraia na Maadili ni mzuri ambapo Maarifa ya Jamii (86.75%) na Uraia na Maadili (85.52%).

"Sayansi ya Jamii, wasichana wana ufaulu mkubwa zaidi kuliko wavulana ambapo somo la Maarifa ya Jamii wasichana wamewazidi wavulana kwa asilimia 1.95 na somo la Uraia na Maadili wasichana wamewazidi wavulana kwa asilimia 1.86," alisema.

Katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, Katibu Mtendaji alisema ufaulu ni wa asilimia 86.86 na somo la Hisabati ni wa asilimia 54, Sayansi na Teknolojia umepanda kwa asilimia 3.67 na Hisabati umepanda kwa asilimia 4.3 kulinganishwa na mwaka 2022.

Alisema somo la Sayansi na Teknolojia wasichana wamefaulu zaidi kuliko wavulana kwa asilimia 1.63 na katika somo la Hisabati wavulana wana ufaulu mkubwa kuliko wasichana, wavulana wana ufaulu wa asilimia 55.4 na wasichana asilimia 52.7.

**KIDATO CHA PILI**

Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi 592,741 kati ya 694,769 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 85.31 wamefaulu kwa kupata madaraja I, II, III na IV. Mwaka 2022 wanafunzi waliofaulu walikuwa 539,645 sawa na asilimia 85.18.

Alisema kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 0.13 pamoja na ongezeko la idadi ya wanafunzi 53,096 sawa na asilimia 9.84 ya wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na Kidato cha Tatu kulinganishwa na mwaka 2022.

"Kati ya wanafunzi waliofaulu kuendelea Kidato cha Tatu, wasichana ni 314,949 sawa na asilimia 83.66 na wavulana ni 277,792 sawa na asilimia 87.28.

"Takwimu zinaonesha wavulana wamefaulu vizuri kulinganishwa na wasichana," alisema.

Dk. Mohamed alisema idadi ya shule katika makundi ya umahiri inaonesha kuwa kati ya shule zote 5,515 zenye matokeo ya upimaji Kidato cha Pili 2023, shule 5,485 sawa na asilimia 98.83 zilipata wastani wa madaraja hayo mwaka 2022.

Hivyo, alisema kumekuwa na ongezeko la asilimia 0.62 la shule zilizopata wastani wa daraja A-D kulinganishwa na mwaka 2022.

Kuhusu ufaulu wa wanafunzi kimasomo, Dk. Mohamed alisema katika masomo ya Sayansi ya Jamii ufaulu wa somo la Historia na Jiografia ni wa wastani. Katika somo la Historia ni wa asilimia 50.71 na Jiografia ni wa asilimia 53.78.

Alisema katika somo la Uraia, ufaulu umeimarika kutoka asilimia 31.12 mwaka 2022 hadi asilimia 48.27 mwaka 2023.

Alisema masomo ya lugha, ufaulu wa somo la Kiswahili na lugha ya Kichina ni mzuri sana ambapo somo la Kiswahili ni asilimia 95.18 na Kichina ni wa asilimia 93.39.

"Masomo ya lugha za Kiingereza na Kifaransa yana ufaulu wa wastani ambapo somo la Kiingereza ufaulu ni asilimia 68.27 na Kifaransa ni asilimia 55.61.

"Aidha, somo la lugha ya Kiarabu ufaulu unaendelea kuimarika kutoka asilimia 47.83 kwa mwaka 2022 hadi asilimia 48.72 kwa mwaka 2023," alisema.

Hata hivyo, Katibu Mtendaji alisema masomo ya lugha za Kichina, Kiarabu na Kifaransa si ya lazima kwa wanafunzi.

Alisema masomo hayo yana idadi ndogo ya wanafunzi ambao ni kati ya wanafunzi 1,921 hadi 10,269 sawa na asilimia kati ya 0.28 hadi asilimia 1.48 ya waliofanya upimaji huo wa kidato cha pili mwaka 2023.

Dk. Mohamed alisema ufaulu masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia, ufaulu wa Bailojia, Uhandisi, Kompyuta, Additional Mathematics na Home Economics ni wa wastani ambao ni kati ya asilimia 55.74 na asilimia 70.29.

Alisema masomo ya Fizikia, Kemia, Kilimo na Hisabati yana ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni kati ya asilimia 19.06 na asilimia 39.24.

Hata hivyo, Katibu Mtendaji huyo alisema ufaulu wa masomo ya Fizikia, Kilimo na Hisababti umepanda kati ya asilimia 0.85 na asilimia 4.52 huku ufaulu wa somo la Kemia ukishuka kwa asilimia 5.29 kulinganishwa na mwaka 2022.

Hata hivyo, Dk. Mohamed alisema Kilimo, Uhandisi, Information and Computer Studies, Additional Mathematics na Home Economics si masomo ya lazima kwa mwanafunzi.

"Masomo haya yana idadi ndogo ya wanafunzi ambayo ni kati ya wanafunzi 441 hadi 27,022 sawa na asilimia 0.06 hadi asilimia 3.91 ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili mwaka 2023," alisema.

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa masomo ya Biashara ni wa wastani; Utamaduni, Sanaa na Michezo ni mzuri, masomo manane ya ufundi ufaulu upo juu ya wastani na katika masomo ya Dini (Bible Knowledge) ni asilimia 84.01 na ufaulu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni asilimia 68.32.

Kuhusu upotoshaji katika mitandao wanaoweka matokeo feki, Katibu Mtendaji huyo alikumbusha kuwa baraza ndilo lenye mamlaka ya kutangaza matokeo huku akisisitiza kuwa, matokeo hayo hayajachelewa kama baadhi ya wadau wanavyodai, hutangazwa siku moja au tatu kabla shule hazijafunguliwa.

Akitolea ufafanuzi waliosajiliwa na hawajafanya mtihani, Dk. Mohamed alisema hilo ni jambo la kitafiti na lina sababu nyingi na kutoa wito kwa wadau washirikiane kwa pamoja kuliangalia tatizo hilo, ili watoto wasiachwe nyuma.

"Ukiangalia takwimu za mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu zinazidi kupungua. Kwanini? Kwa sababu uelewa katika jamii umezidi kuongezwa na usajili wa wanafunzi umeongezeka," alisema.

Kuhusu watoto waliopata mimba na kurejeshwa shuleni, alisema watashirikiana na mamlaka husika kuziomba taarifa, lakini taarifa za usajili wa mtahiniwa huwa wawaweki hicho kipengele.

HABARI KITAIFA

MUSWADA SHERIA YA UCHAGUZI

# Askofu Shoo: Serikali iheshimu maoni ya wadau

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo (pichani), ametoa wito kwa serikali kuyaheshimu na kuyafanyia kazi maoni yanayotolewa na wadau wakiwamo viongozi wa dini kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi.

Pia amesisitiza wabunge kuyafanyia kazi mambo ambayo yamekuwa yanalalamikiwa mara kwa mara na wadau wa siasa ikiwamo kuundwa Tume Huru ya Uchaguzi.

Dk. Shoo alitoa wito huo jana wakati akiongoza ibada maalum ya kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini Askofu Mteule Dk. Antony Kipangula na Msaidizi wa Askofu, Kefa Ulula iliyofanyika katika Kanisa la KKKT Usharika wa Mafinga, Dayosisi ya Mufindi.

Akitoa neno katika ibada hiyo, Dk. Shoo alisisitiza serikali kuwa upokeaji maoni hayo ufanyike kwa dhati na umakini mkubwa kwa kuzingatia weledi ili kujenga Tanzania yenye amani, mshikamano na maridhiano kama watakavyo Watanzania.

Pia aliwasisitiza wabunge kuchukua nafasi zao kama wawakilishi wa wananchi wakiwawakilisha katika mchakato huo wa mabadiliko ya sheria hiyo.

"Tunataka Tanzania ambayo ina amani, mshikamano, maridhiano. Tanzania ambayo Watanzania wakitoa maoni yao kwa kile wanachotamani nchi yao iwe kiheshimiwe," alisema Dk. Shoo.

Kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi, Dk. Shoo alikumbusha wabunge kulifanyia kazi suala hilo kwa kuwa limekuwa hitaji la Watanzania wengi.

Alisema anafurahi kuona wadau mbalimbali ikiwamo vyombo vya dini kupewa mwaliko wa kutoa maoni yao kuhusiana na sheria hiyo na wanaendelea kutoa kwa maslahi mapana ya taifa.

Kiongozi huyo wa kanisa alishukuru wadau mbalimbali walioshirikishwa katika utoaji maoni hayo, akisema wao kama viongozi wa dini walipoalikwa na baraza walitoa maoni na wataendelea kufanya hivyo kila wakati watakapohitajika.

Alisema anamshukuru Mungu kwa kuwapa Rais anayetambua mchango wa vyombo vya dini, kwamba hajawahi kuwaacha wakati wowote wanapomwalika.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera - Bunge na Uratibu, Jestina Mhagama, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alisema analishukuru kanisa hilo kwa kuendelea kufanya kazi kwa pamoja katika kuhudumia Watanzania.

Alitolea mfano kuwa katika maafa ya Hangang, kanisa hilo lilitoa wataalamu wa saikolojia kwa ajili ya kutoa tiba ya kisaikolojia kwa waathirika wa maafa hayo.



Pia alipongeza kanisa hilo kwa kuanzisha dayosisi hiyo, akisema ni ishara inayoonesha kuwa eneo hilo limekuwa kiuchumi, kimaadili na shughuli za kijamii.

"Kitendo cha KKKT kuanzisha eneo la kiutawala ambalo ni la dini si jambo la kawaida, sisi kwetu ndani ya serikali tukiongozwa na Rais tunatizama jambo hili kwa jicho lingine, tunaona kuna msukumo mkubwa wa utashi, weledi, uzalendo ambao utakuwa ni chemchemi ya maendeleo ya taifa," alisema Jestina.

Alisema kukua kwa imani katika jamii kuna mchango mkubwa wa ukuaji maendeleo endelevu ya taifa hasa katika kipindi hiki ambacho kuna ukuaji wa sayansi na teknolojia unaochochea mmomonyoko wa maadili.

Waziri Jenista alisema kukua kwa kanisa kutachochea maadili, kupambana na rushwa, kuimarisha utawala bora, kuweka misingi ya maendeleo, hivyo nchi kupiga hatua kiuchumi.

Aliwataka waumini wa dayosisi hiyo kuwatii viongozi wao wa dini kwa kuwa wamepewa dhamana ya kuwaongoza kiroho, hivyo wanapaswa kwenda kujenga umoja na upendo kama familia.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria imeanza rasmi kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Muswada wa Sheria wa Vyama vya Siasa ya Mwaka 2023.

Miswada hiyo ilifikishwa bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza Novemba 10, mwaka jana na sasa kamati hiyo itasikiliza na kupokea maoni kwa muda wa siku tatu hadi Januari 10, mwaka huu.


## Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationships beyond banking*

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions) (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

A. REMITTANCE –OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

B. REMITTANCE –INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

D. Other Common Charges

| Item | Charges TZS A/c | Charges USD A/c |
|---|---|---|
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees TZS A/c | Charge/Fees USD A/c |
|---|---|---|
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

CREDIT MATTERS

| | Charge/Fees |
|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher. |
| | **Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>2) **Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** |

**D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)**

| | USD Facility | TZS Facility |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD 5 | TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

**Guarantee (Performance/Financial) :-**

| | |
|---|---|
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

**OTHER DISCLOSURES**
**(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 27.12.2023 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 27.12.2023 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 27.12.2023 |

177676

MAZUNGUMZO MAALUM

# Kilichojificha ndege kukosa kiti namba 13

## -Rubani ataja kinachompa kesi ya kujibu mahakamani, wajawazito kuzuiwa...

**Na Christina Mwakangale**

NARSCENT Meena (pichani) ni rubani. Kwake kuwa angani kwenye mawingu tulivu, huifanya siku yake kuwa njema. Hana hofu anapokuwa angani.

Licha ya wazazi wake kutamani awe daktari wa binadamu kutokana na matokeo mazuri ya kidato cha nne, alibaki na ndoto ya kuwa rubani.

Rubani huyo pia anatoa ufafanuzi kuhusu ndege kutokuwa na kiti namba 13 katika utaratibu wa maalum wa safu, akibainisha kuwa kunatokana na imani kwamba namba hiyo ina shida, ni namba hatari kuliko zote katika usafiri huo.

"Ndege nyingi hazina kiti namba 13. Ninajua ni jambo la kuwashangaza wengi. Mfano, ndege Aina ya ATR 72 au ATR 42 hazina kiti namba 13.

"Na baadhi ya ndege nyingine kubwa hutoka kiwandani na kiti namba 13, lakini mashirika ya ndege huagiza kuziondoa," anasema Narscent.

Rubaini huyo anasema mashirika ya kimataifa ambayo hufanya safari kubwa kwenda bara moja hadi lingine, yana utaratibu huo na kwamba zipo ndege zingine pia huiondoa safu ya namba 17, wakiungana na imani ya kile kinachoikumba namba 13.

"Sababu kubwa ni imani kwamba namba 13 si namba ya bahati," rubani huyo anasema.

Kwa mujibu wa tovuti ya euronews. travel, hofu ya kiti hicho ni maarufu kwa safari za ndege na imepewa jina la 'triskaidekaphobia' na hofu hiyo ilianza mwaka 1911 huko Marekani kwenye kitabu kilichoandika kuhusu saikolojia.

Inaelezwa katika tovuti hiyo kuwa namna namba 13 ilivyo na bahati mbaya kwenye kitabu kitakatifu cha Biblia ni kwamba hata Yuda Iscariot aliyemsaliti Yesu, alikuwa mgeni wa 13 wakati wa karamu ya mwisho, yaani mlo wa jioni.

Pia inaelezwa katika tovuti ya simpleflying.com kwamba si katika ndege tu namba 13 inaogopwa, bali pia katika hoteli nyingi hazina chumba namba 13; majengo marefu hayana ghorofa ya 13, wakishafika ghorofa ya 12, inayofuata ni ghorofa namba 14.

Inaelezwa katika tovuti hiyo kuwa utafiti uliofanywa Gallup mwaka 2007, ulibaini asilimia 13 ya wageni hawataki kupewa chumba kilichoko ghorofa ya 13 katika hoteli za Amerika.

Narscent (30) alisoma Shule ya Sekondari Jitegemee kisha akajiunga Shule ye Sekondari Tambaza, mkoani Dar es Salaam alikosoma kidato cha tano na sita, lakini hakufanya vizuri katika mtihani wa kidato cha sita, hivyo alikaa nyumbani kwa miaka miwili bila shughuli yoyote.

Alianza masomo ya urubani, akijilipia ada aliyoikusanya kwa muda mrefu na alipohitimu masomo ya huduma katika ndege, akifanya kazi kwa miezi minne pekee, alifanikiwa kuweka akiba ya Sh. milioni nne.

"Watu walinichangia nilifikisha Sh. milioni 19, nikaenda chuo kwa miezi 14, chuo kiitwacho Sunquest Aviation, kipo Johannesburg, Germiston Town, Rand Airport Hangar No. 4, nchini Afrika Kusini.

"Nimehitimu Aprili 26, mwaka huu (2023). Aprili 26 kila mwaka ni Siku ya Marubani Duniani, hivyo ni fahari kuhitimu siku hiyo kwa kufaulu mtihani wangu wa mwisho.

"Kwa sasa nina leseni ya rubani. Masomo ya sayansi yanasaidia kukupa uelewa katika ndege," anaeleza Narsent katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam.



**Swali: Kipi kilikusukuma kusomea fani hii?**

**Jibu:** Nilichagua hii kazi kwa sababu niliona nina kitu cha tofauti ambacho tasnia ya anga inakikosa na jamii inayonizunguka inakikosa pia. Hivyo, nia yangu haikuwa kuwa rubani wa ndege tu, bali rubani wa jamii inayonizunguka. Nikiwaleta vijana wengi na jamii nzima karibu na tasnia ya anga.

**Swali: Kwanini ndege kubwa rubani huwa katika chumba binafsi na hizi ndogo abiria wanamwona?**

**Jibu:** Ni suala la usalama, hasa hizi ndege za kisasa, zina vyumba vya marubani vinavyofunga kwa sababu ya matukio mengi ambayo yamewahi kutokea huko nyuma.

Kwa ndege ndogo nyingi ni za zamani na nyingine zina zaidi ya miaka 50 iliyopita. Wakati huo hakukuwa na matukio hayo ya utekaji wa ndege kama ambavyo yamekuwa yanaongezeka. Ninajua utauliza 'kama ni hivyo kwanini bado zinatumika?'

Kwa Tanzania yetu ni salama sana kwa kuwa ndege nyingi ndogo zinafanya safari za ndani kwa ndani na chache zinakwenda nchi jirani. Ninaamini ndio maana zinaendelea kutumika mpaka leo. Kama usalama ungekuwa mdogo, basi ninaamini zisingekuwa zinatumika kabisa.

Kwa ndege kubwa, watu ni wengi na wanatoka sehemu mbalimbali na nia zao ni tofauti. **Swali: Ni wakati upi rubani hufanya mawasiliano akiwa kwenye ndege?**

**Jibu:** Rubani hufanya mawasiliano kabla ya kuruka na wakati wa kutua ili kujua njia gani anapaswa kutumia ili kufika kwenye barabara ya kukimbia kwa kasi ili kuruka.

Kuepusha ajali mbalimbali wakati wa kuruka, kwa kuwa namna ndege inavyopishana na ndege nyingine si kama gari. Kuna utaratibu wake na hesabu huhusika ili kufanikisha mruko.

Mawasiliano si wakati wa kuruka na kutua tu, hata ndege ikiwa angani, sisi huwa tunawasiliana na ndege nyingine kupitia masafa husika.

**Swali: Rubani ni miongoni mwa kazi zinazopewa hadhi kubwa katika jamii. Unaichukuliaje dhana hiyo?**

**Jibu:** Kwa upande wangu ninaichukulia kama kazi zingine na ninaipenda kama watu wengine wanavyopenda kazi zao. Utofauti ni mitazamo yetu tu katika hii kazi.

Kwangu ni fursa ya kuelimisha jamii kama ambavyo nimekuwa ninafanya, ili ile mitazamo ambayo si ya kweli iondoke miongoni mwa jamii inayonizunguka.

**Swali: Ni zipi dalili hatari unapokuwa angani?**

**Jibu:** Injini ya ndege kufeli, injini kupata moto, kuingia kwenye mawingu hatarishi, hizo ni chache. Iliyowahi kunikuta ni kuingia kwenye mawingu makubwa na nikawa sioni mbele wala nyuma na nilikuwa niko peke yangu.

Hii ilisababishwa na mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa amabayo sikuwa nimeyaona kwenye 'forecast' (utabiri wa hali ya hewa).

Nimekuwa kwenye tasnia ya anga kwa takribani miaka 10 sasa. Yaani nimewahi kuwa mhudumu wa kwenye ndege, yaani (flight attendant/cabin crew).

Hivyo basi, niko ninafanya changizo kwa mtu mmoja mmoja na pia nimeiomba serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili kwenda kumalizia hatua ya mwisho ya CPL (Commercial Pilot License) ili nije kulitumikia taifa langu kwa ndege zetu za Air Tanzania.

Nimeweza kufika hapa kwa michango ya Watanzania wenzangu na juhudi binafsi ikiwamo kuuza karanga. Gharama ya kusoma urubaini inaweza kufika wastani wa Sh. milioni 130 mpaka kumaliza CPL. Bado sijafika ninakotamani kufika, ila siko mbali kufika.

**Swali: Ni vigezo gani vya kujiunga na masomo ya urubani?**

**Jibu**: Kigezo kikubwa ni kufaulu kidato cha nne. Shule nyingi za urubani duniani zinapokea kuanzia hiyo ngazi kwenda juu.

Kwa kuongezea, kigezo cha kimo kilikuwapo zamani, ila kwa sasa hakitumiki tena. Hiki kigezo kinatumika zaidi kwa wahudumu kwenye ndege.

**Swali: Wahudumu wa ndege huwa na tabasamu, wakarimu muda wote. Ni kwa sababu ya mshahara mnono au kuna lingine?**

**Jibu:** ... (kicheko) Hapana! Si sababu ya mshahara mnono. Huduma nzuri kwa wateja ni jambo muhimu sana kwenye tasnia ya anga hususani uhudumu. Hivyo, hata wale wasioweza kutabasamu lazima wajifunze kufanya hivyo.

Marubani si wote, hapa huwa ukarimu unakuja kama tabia ya mtu hasa kwa marubani kwa kuwa wao hawana uhusiano wa moja kwa moja na abiria.

**Swali: Inapotokea dharura ukoaji huchukua dakika ngapi na mlango wa dharura huko angani unafunguka?**

**Jibu:** Inapotokea dharura, mlango wa ndege huwa haufunguliwi angani. Mara nyingi dharura ikitokea, ni kuelekeza ndege kwenye uwanja ulio karibu au kama hakuna uwanja huwa ni bahari au ziwa. Iwapo ndege ikitua kwenye maji, uokoaji unatakiwa kufanyika ndani ya sekunde 90.

**Swali: Tumesikia tangu wadogo kwamba hewa kuingia kwenye ndege ni hatari kubwa zaidi. Kuna ukweli katika hili?**

**Jibu:** Ni kweli hewa kuingia ndani ya ndege ni hatari. Hasa zile ndege zinazoruka umbali mrefu zaidi. Yaani unaweza kuchukua mfano wa mpira wa miguu unapotoboka. Ndivyo ambavyo ndege inavyoingiza upepo inavyokuwa.

Hili jambo haliathiri sana ndege ndogo kama zile kubwa, kwani zenyewe haziruki umbali mrefu kutoka usawa wa bahari.

**Swali: Kwanini abiria afunge mkanda ndege inapopaa na kutua?**

**Jibu:** Abiria hufunga mkanda kwa sababu ya usalama, kama ilivyo kwenye gari, vivyo hivyo kwenye ndege. Pia kwa kuongeza huwa inashauriwa kufunga wakati wote kwa sababu ya mitikisiko ya ghafla ambayo inaweza kutokea huko angani.

Mawingu yanaweza kuathiri kasi ya mwendo hata kubadilisha hali ya hewa kwa ujumla. Kuna mawingu ya chini ya kati na ya juu kabisa, pia yapo mawingu hatari kama wingu linaloitwa Cumulonimbus.

Ndege ndogo inaweza kufika urefu wa futi 11,000 kutoka usawa wa bahari. Kwa ndege kubwa huweza kufika hadi wa futi 39,000 na hata futi 41,000.

**Swali: Kanuni ya abiria hawa; watoto na wajawazito ikoje ndani ya ndege?**

**Jibu:** Swali zuri sana. Kwa utaratibu wa ndege, sisi mtoto mwenye umri wa miaka 0-1 ni (infant) hata kwenye kusafiri uzito wake huunganishwa na ule wa mama yake.

Kuanzia miaka miwili kwenda juu ndio anakuwa (child). Yaani hapa mtoto analazimika kupata kiti chake kwenye ndege.

Kwa suala la mjamzito, mimba ikishapita wiki 35 anapaswa kuwa na kibali kutoka kwa daktari kwa kuwa 'complications' zinaweza kutokea mara nyingi kuanzia wiki ya 36. Bila kibali anaweza kuzuiliwa kusafiri.

**Swali: Je, ni kweli rubani hulipwa kila anapofanya safari moja?**

**Jibu:** ....(kicheko) Sisi tuna mkataba kama zilivyo kampuni zingine na tunalipwa mwisho wa mwezi. Na suala la kulipwa kila safari ndio lipo, ni posho ndogo ambazo zimewekwa na kampuni za ndege.

Kama kampuni za kawaida zilivyo na marupurupu basi na sisi ni hivyo, inawezekana kwetu ikawa tofauti kidogo ila haiko mbali na ile maana ya marupurupu.

**Swali: Kwanini ndege hupita pembezoni mwa bahari au ajali ikitokea nyingi huangukia majini?**

**Jibu:** Si kwamba ndege hupita pembezoni mwa bahari. Ndege zina njia zake ambazo ni za kufikirika ambazo zimewekwa na wataalamu.

Ikitokea ajali rubani anapaswa kuwa wa mwisho kutoka. Rubani anapaswa kujiokoa tu pale ambapo anaona maisha yake yapo hatarini.

Ikitokea rubani amejiokoa na kukawa na abiria kwenye ndege ambao nao walijiokoa baada ya yeye kujiokoa, kisheria ana kesi ya kujibu.

Maana ya kuwa rubani ni kuwa kiongozi na kiongozi kazi yake ni kuhakikisha watu wake ni salama.

**Swali: Kwanini mnavaa shati jeupe na hizo nembo mabegani zina maana gani?**

**Jibu:** Ni swali zuri. Urubani umezaliwa kutoka jeshini. Kwa hiyo, unadhifu unaonekana jeshini, ndio zao kubwa la marubani. Hizo 'bars' za mabegani na sare kwa ujumla ndio heshima ya urubani wenyewe.

Wale waanzilishi waliona vyema iwe hivyo na sisi tunapenda na kufuata kile kilichoanzishwa, huku tukiiona fahari ya vazi.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi aahidi wawekezaji usalama wa miradi yao

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaahidi wawekezaji wote visiwani humo kujenga imani kuwa miradi yao ipo salama na italindwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana alipoweka jiwe la msingi la hoteli yenye hadhi ya nyota tano ya 'Zanzibar Crown' ya mwekezaji kutoka Oman yenye thamani ya Sh. bilioni 50.

Alisema kasi ya miradi ya uwekezaji katika hoteli za kimataifa inadhihirisha kwamba Zanzibar ipo salama na amani na utulivu vimeimarishwa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kuweka sheria ambayo itawahakikishia wawekezaji hao miradi yao kuwa salama zaidi.

Alisema sheria mpya ya Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA) imewasamehe kodi wawekezaji wa kimkakati kwa zaidi ya miaka 15 na mamlaka hiyo kuwa bora zaidi katika uwekezaji.

"Sheria mpya ya uwekezaji ya mwaka 2023 tayari ipo mezani kwangu ambapo tumetayarisha siku maalumu kwa ajili ya kutia saini na kufanya sherehe kubwa na hii itaifanya ZIPA kuwa taasisi bora zaidi katika Bara la Afrika," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Hussein Ali Mwinyi katika uwekezaji na jumla ya miradi 266 imewekezwa hadi kufikia Novemba mwaka 2023.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na ZIPA kwa sasa ni kujenga mazingira mazuri ambayo yatawahakikishia wawekezaji ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, umeme na majisafi na salama.

Aidha, ujenzi wa barabara inayokwenda katika maeneo ya uwekezaji Micheweni yenye urefu wa kilomita 13 imekamilika ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuwavutia wawekezaji.

"Mheshimiwa kasi ya uwekezaji inaendelea kwa kiwango kikubwa ambapo kituo cha uwekezaji ZIPA kinafanya kazi kubwa ya kutangaza fursa za uwekezaji nchini," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uwekezaji na Uchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema mageuzi makubwa yaliyofanywa katika mamlaka ya vitega uchumi ZIPA ikiwamo marekebisho ya sheria kwa kiasi kikubwa yamesaidia wawekezaji kuja nchini kuwekeza.

Alivitaja vivutio hivyo ni kukifanya kituo cha ZIPA kuwa kimoja kwa ajili ya shughuli za uwekezaji 'One Stop Center' kwa mwekezaji wa kimkakati kusamehewa kodi kwa muda wa miaka 15.

Balozi Mdogo wa Oman, Said Salim Al-Sinawy, alisema amefurahishwa na mabadiliko makubwa yanayofanywa na Serikali ya Zanzibar katika uwekezaji kwa kuweka sheria bora zinazowalinda wawekezaji.

"Mheshimiwa katika kipindi cha miaka mitatu umejenga mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo yanawahakikishia wawekezaji miradi yao kuwa salama," alisema.

Mwekezaji Nadhim Mohamed, alisema mradi huo unatarajia kutoa ajira za wafanyakazi 200 huku akivutiwa na mazingira mazuri yenye uwazi zaidi.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akipokewa na Kwaya ya Makuburi katika harambee ya kuchangia ujenzi wa Kituo cha Huduma cha Masista wa Shirika la Dada Wadogo Mtakatifu Francisko kinachotarajiwa kujengwa Bagamoyo. Harambee hiyo imefanyika ukumbi wa Marantal Msimbazi Centre jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima korosho kulipwa mabilioni

Na Mwandishi Wetu, TUNDURU

WAKULIMA wa korosho katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma wanaohudumiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma (TAMCU), wamevuka lengo la uzalishaji wa zao hilo katika msimu wa kilimo 2023/24.

Ni baada ya kufanikiwa kuzalisha na kuuza jumla ya tani 26,066 zenye thamani ya Sh. bilioni 45.531.

Hilo ni ongezeko la tani 1,000 kulinganisha na msimu uliopita ambao walizalisha tani 25,000.

Kaimu Meneja wa TAMCU, Marcelino Mrope, alibainisha hayo jana alipozungumza na wanachama wa Chama cha Msingi cha Ushirika Ligunga (Ligunga Amcos) katika mnada wa nane na wa mwisho katika msimu wa kilimo wa 2023/24.

Mrope alisema hayo ni mafanikio makubwa kwa wakulima na chama hicho katika uzalishaji korosho, akiwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya mashambani kwa mwaka 2023/24.

Alishukuru serikali kwa kutoa pembejeo za kilimo bila malipo kwa wakulima, hali iliyohamasisha wakulima wengi kurudi mashambani kwa ajili ya kufufua mashamba yao.

"Kwa mfano, katika msimu huu wa kilimo tumepewa pembejeo zenye thamani ya Sh. bilioni 22.5, kitu ambacho hakijawahi kutokea tangu nchi ipate Uhuru.

Tunaamini pembejeo hizi zitakwenda kuongeza sana uzalishaji korosho katika wilaya yetu," alisema Mrope.

Aliwashauri wakulima kutumia vizuri fedha walizopata kununua pembejeo na kutumia mvua iliyoanza kunyesha kuanza maandalizi ya msimu mpya wa kilimo.

Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule alisema bei ya korosho msimu wa mwaka huu haikuwa nzuri kulinganisha na msimu uliopita, lakini akawataka wakulima kutokatishwa tamaa badala yake waendelee kulima zao hilo ambalo ni nguzo kuu ya uchumi wao na Wilaya ya Tunduru.

Manjaule alitoa ushauri kwa wakulima kuanza kulima mazao mengine ya chakula na biashara ikiwamo mbaazi zenye soko la uhakika na bei kubwa na halihitaji gharama kubwa katika uzalishaji wake.

Ofisa Ushirika wa wilaya hiyo, George Bissan, alipongeza Bodi ya TAMCU kwa kusimamia vyema mauzo ya korosho kwa mfumo wa stakabadhi ghalani ambao umewezesha wakulima kuwa na soko la uhakika na kupata fedha zao kwa wakati.

Aliwaasa wakulima kutumia fedha walizopata kufanya mambo ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa nyumba bora, kusomesha watoto na kuanzisha shughuli nyingine zitakazowaingizia kipato badala ya kutumia fedha hizo kwenye ulevi na uwasherati.

Rashid Millanzi, mkulima wa korosho, aliipongeza serikali kupitia TAMCU kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani.

Hata hivyo, mkulima huyo aliomba kutafuta wafanyabiasha wengi watakaokwenda kununua korosho kwa bei nzuri inayolingana na gharama za uzalishaji wake.

# Jafo: Wazanzibar wanastahili kujivunia maendeleo muda mfupi

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema wananchi wa Zanzibar wanastahili kujivunia maendeleo yaliyopatikana kwa muda mfupi.

Aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hoteli ya Kiwengwa Tembo Beach iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Dk. Jafo alisema kuwa uwekezaji wa miradi ikiwamo afya, elimu, miundombinu na uwanja wa ndege unaofanyika chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ni fursa kubwa kwa wananchi ambayo inawaletea kipato pamoja na kukuza uchumi.

Alisema viongozi hao wakuu wa serikali hizo mbili pia wameonesha dhamira ya kuifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na mapinduzi ya viwanda ambavyo ni sehemu ya uwekezaji na kukuza uchumi.

Dk. Jafo alisema viongozi wamefungua milango ya uwekezaji mkubwa wa ndani na nje ya nchi kwa kujenga na kuimarisha miundombinu muhimu itakayoweza kutoa fursa za kimaendeleo kwa wananchi.

Pamoja na mambo mengine, Dk. Jafo alitoa wito kwa wawekezaji nchini kuzingatia uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoikabili dunia.

Alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa sekta zinazoingiza mapato hasa utalii kwa hiyo ni wajibu wa kila mmoja kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuhifadhi mazingira zikiwamo kupanda miti.

Vilevile, alitoa wito kwa wananchi kutunza na kusafisha fukwe zilizopo katika maeneo mbalimbali ili ziwe katika mazingira safi na ya kuvutia ikiwa ni sehemu ya kukuza uchumi wa buluu kama unavyochagizwa na serikali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili Klabu Ligi Kuu uzingatie muda wa dirisha wanaoachwa

**ZIMEBAKI** siku takribani nane kabla ya dirisha dogo la usajili Tanzania Bara kufungwa rasmi Januari 16, mwaka huu baada ya kufunguliwa Desemba 16, mwaka jana, kwa klabu zote za Ligi Kuu, Championship na zile za First League.

Kama inavyofahamika, dirisha hilo ni maalum kwa klabu kuziba mapengo yaliyojitokeza raundi ya kwanza na kujiimarisha kuelekea mzunguko wa pili, ingawa bado raundi ya kwanza ilikuwa haijamalizika kutokana na sababu mbalimbalii zilizoainishwa kwa nyakati tofauti na Bodi ya Ligi nchini, TPLB.

Moja ya sababu awali ikiwa ni kuanzishwa kwa michuano mipya ya African Football League (AFL), ambayo kwa Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki kwa ujumla, Simba pekee ndiyo iliyokuwa ikishiriki, hivyo kusababisha baadhi ya mechi kusimama.

Lakini pia kwa sasa ligi hiyo ikisimama kupisha Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zinazotarajiwa kuanza Jumamosi wiki nchini Ivory Coast huku Tanzania ikitarajiwa kutupa karata yake ya kwanza Januari 17, mwaka huu dhidi ya Morocco.

Hata hivyo, katika kipindi hiki fainali hizo zikiendelea pia ni muda wa usajili wa dirisha dogo na tayari klabu mbalimbali zimeaza kutangaza nyota wao wapya, ambao baadhi wameanza kuzitumikia katika michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea visiwani Zanzibar.

Azam FC, Simba, Singida Fountain Gate na Yanga ni miongoni mwa timu kutoka Tanzania Bara zinazoshiriki michuano hiyo na baadhi ya wachezaji wao waliosajili katika dirisha hili wameonekana wakizitumikia kwenye mashindano hayo.

Hata hivyo, hakuna klabu yoyote kati ya hizo ambayo imetangaza wachezaji itakaoachana nao ama kuwatoa kwa mkopo licha ya kutangaza waliowasajili na kuanza kiwatumia katika michuano hiyo ambayo kanuni huruhusu hata wale wa majaribio kutumika.

Hivyo, tunatamani kuona kasi hiyo ya usajili ikienda sambamba na wale wanaowatema ama kuwatoa kwa mkopo ili kuwapa fursa na uhuru wakutafuta malisho kwingineko kabla ya dirisha kufungwa wiki ijayo.

Tunatambua zipo klabu nje ya Azam FC, Simba, Yanga na Singida Fountain Gate, ambazo zinavizia wachezaji watakaotemwa ama waliopo kwenye orodha ya kutolewa kwa mkopo, ili wawasajili, hiyo ikitokana na kutokuwa na uwezo wa kwenda kuvunja mikataba yao kuwanunua.

Kwa muktadha huo, kwa kuwa mpira ni maisha yao, tunaona itakuwa vema na busara kwa klabu hizo na nyingine zote zinazohusika katika usajili huu wa dirisha dogo kuwatangaza mapema wanaopewa mkono wa kwaheri ili kutoa nafasi kwao kuchagua klabu zinazowafaa na kwa maslahi sahihi badala ya kusubiri siku za mwisho kabla ya dirisha kufungwa.

Lakini pia ni wakati sahihi kwa wachezaji ambao nafasi zao za kucheza ni finyu na wale wasiopata kabisa, kuomba kuondoka ama kutolewa kwa mkopo ili kulinda vipaji vyao badala ya kuendelea kusubiri dakika za mwisho jambo ambalo linaweza kuwasababisha kupata timu isiyo chaguo lake.

Haina maana kwa mchezaji ambaye hadi sasa ligi ikielekea raundi ya pili, haujapata nafasi angalau mechi mbili, halafu aendelee kusubiri, badala ya kuomba kuondoka ili kwenda kulinda kipaji chake.

Mwisho, tunatambua gharama kubwa ambazo klabu zitakabiliwa nazo endapo zitavunja mkataba na mchezaji na hicho ndicho kikwazo kikubwa kwa sasa, hivyo tutoe rai kwa wachezaji ambao hawapati nafasi kikosini kuona umuhimu wa kukaa meza moja na klabu zao kurahisisha mambo ili kwenda kulinda vipaji vyao.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Maandalizi Klabu Ligi Kuu ni sasa, visingizio havitakuwa na maana

Na Adam Fungamwango

**MECHI** za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa zimesimama kwa ajili ya kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi na Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 zinazotarajiwa kuanza kupigwa Jumamosi nchini Ivory Coast.

Ni Ligi ya Championship, Ligi Daraja la Pili, 'First League', na ya wanawake ndizo zinazoendelea kuchezwa nchini.

Kwa mujibu wa kalenda ya Bodi ya Ligi, ni kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara itaanza tena kutimua vumbi Februari 16 na baada ya hapo mechi zingine za viporo zitapachikwa baadaye katika siku ambazo zitaonekana kuna nafasi ya kufanya hivyo.

Mara ya mwisho kuchezwa mechi za Ligi Kuu ilikuwa ni Desemba 23, mwaka jana hivyo kwa haraka haraka unaweza kuona kuna kiasi cha miezi miwili ambayo klabu zimepumzika.

Hata hivyo, kuna baadhi ya timu nne ambazo ni Simba, Yanga, Singida Fountain Gate, Azam FC zipo kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, hivyo wachezaji wao bado wanaendelea kufanya mazoezi na kucheza soka.

Pia timu hizo zina baadhi ya wachezaji kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars pamoja na mataifa mengine watakaokipiga katika michuano ya AFCON.

Hapa unaweza kuona kuwa pamoja na kwamba kuna mapumziko ya kiasi cha miezi miwili, lakini timu hizo hazitoathirika sana kwani wachezaji wao wengi bado watakuwa na utimamu wa mwili kabla ya kurejea kwenye Ligi Kuu.

> **Hapa unaweza kuona kuwa pamoja na kwamba kuna mapumziko ya kiasi cha miezi miwili, lakini timu hizo hazitoathirika sana kwani wachezaji wao wengi bado watakuwa na utimamu wa mwili kabla ya kurejea kwenye Ligi Kuu.**

Tatizo naliona kwenye timu zingine zilizobaki, kwani zimekuwa kimya mno na taarifa zinasema nyingi zimewaruhusu wachezaji wao kwenda majumbani mpaka hapo watakapotangaziwa tena.

Najua wakati mwingine hili linafanywa kwa sababu ya ukata, yaani viongozi wa klabu wanawaruhusu wachezaji na kuwarudisha wiki moja tu kabla ya ligi kuanza.

Hakuna asiyetambua kuwa ukiondoa klabu za majeshi na zile kubwa na kongwe, zilizobaki zina matatizo ya kifedha, hivyo kuwaita wachezaji wake siku chache kabla ya ligi kuanza ni kubana matumizi. Hatukatai hilo, lakini hatuhitaji malalamiko mbele ya safari kuwa muda wa kujiandaa ulikuwa mdogo.

Baadhi ya makocha wanapopoteza mechi mara nyingine wamekuwa wakilalamikia ufinyu wa muda wa kuwakusanya wachezaji, kuwaandaa.

Nadhani huu ndiyo muda wa makocha kuwahimiza viongozi wao kutafuta pesa kwa ajili ya kuanza mapema maandalizi ya ligi kuliko kuanza kuwalalamikia watu wengine baadaye.

Hakuna timu inayoweza kufanya vizuri ikiwa na wachezaji ambao wana wiki moja tu tangu waanze mazoezi, kwenda kucheza na timu ambazo zilikuwa zinakipiga kipindi kirefu cha mapumziko.

Inakutana na timu yenye wachezaji wenye pumzi na stamina waliotoka Kombe la Mapinduzi, waliotoka kucheza AFCON, huku yenyewe ikiwa na wachezaji waliotoka nyumbani, hawawezi kufanya vizuri.

Mashabiki wengi wa soka huwa wanapenda ushindani kwenye Ligi Kuu, hata kama timu inafungwa, lakini ionekana imepambana vya kutosha na si kuonekana kama mechi ya timu zenye madaraja tofauti.

Februari si mbali, huu ni wakati wa timu za Ligi Kuu kuanza sasa kukusanya wachezaji, waanze mazoezi kabla ya kuingia kambini kwa ajili ya kukabiliana na timu si zenye uchumi mzuri tu, lakini pia zenye wachezaji ambao bado wako fiti kwa kupumzika kipindi kifupi tu.

Kuna timu zipo chini ya msimamo, hakuna uchawi mwingine wa kuondoka huko kama maandalizi hayatoanza mapema. Ni kweli zinafanya usajili kipindi hiki, lakini bila mazoezi ya mapema yenye tija bado hakuna kitu.

Maandalizi ni sasa, baada ya hapa hakutokuwa tena na muda wa kujiandaa kwani itakuwa ni mechi mfululizo, malalamiko yatakuwa ni kazi bure tu.

# Vijiji 90 vyapatiwa baiskeli kurahisisha utoaji huduma

**Na Said Hamdani,**
LINDI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewapiga jeki watendaji wa vijiji 90 kwa kuwapatia vyombo vya usafiri ili kutekeleza majukumu ya kuhudumia jamii katika maeneo yao.

Usafiri huo ni baiskeli zilizotolewa kwa watendaji wa vijiji husika wilayani humo kuwapunguzia tatizo la kutembea kwa miguu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akikabidhi baiskeli 70 kati ya 90 kwa vijiji hivyo, Waziri Mkuu aliwataka watendaji kuzitunza na kuzitumia kwa uangalifu ikiwa ni pamoja na kuzifanyia matengenezo zinapoharibika ziweze kumudu kwa muda mrefu.

"Nilipoona wenzenu wa kata, tarafa na maofisa kilimo wamepewa pikipiki nikaona na nyinyi mpatiwe angalau hizi baiskeli," alisema.

Wilaya ya Ruangwa yenye vijiji visivyopungua 90 watendaji wake walikuwa na mazingira magumu ya kutembea kwa miguu wanapotekeleza shughuli zao za kazi kutokana na kukosa usafiri.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa usafiri huo, watendaji Juma Issa, Daudi Selemani, Mwanaisha Yusufu na Mgeni Mohamedi wamemshukuru Waziri Mkuu ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kuwakumbuka kuwapatia usafiri huo ambao utasaidia kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao tofauti na ilivyokuwa hapo awali.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akiomba dua katika kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume lililopo Kisiwandui, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko akumbusha matumizi rasilimali kwa maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameitaka Jumuiya ya Wazazi ya CCM kutumia rasilimali walizonazo kukijenga na kukieneza Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuzungumza na wananchi kuhusu kazi kubwa za maendeleo zinazofanywa chini ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Dk. Biteko ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (Kundi la Wazazi), amesema hayo wakati akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM-Zanzibar wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Dogo Mabrouk. Kikao kilifanyika katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

"Kama wewe ni mwenyekiti wa mkoa, katibu wa mkoa au kiongozi yeyote yule kwa kutumia rasilimali ulizonazo tembelea maeneo ya mkoa wako, wilaya na vijiji hata mara moja, zungumza na makundi mbalimbali ikiwamo wajumbe wa kamati za utekelezaji za jumuiya yetu na waeleze kuhusu masuala ya kujenga na kueneza chama. Hii inawezekana, tujipange, tufanye ziara hata kama ni kidogo, polepole tutafanya makubwa kadri tutakavyoendelea, tuwe mstari wa mbele kueleza mafanikio ambayo CCM na serikali yake wameyafanya," alisisitiza Dk. Biteko.

Alisema, Jumuiya ya Wazazi ya CCM ni kubwa ndani ya chama inapaswa kufanya kazi za kukijenga kwa ukubwa huo kwa kuwa inabeba makundi yote na haina mipaka au ukomo wa mtu kuwa sehemu ya jumuiya.

"Nikitolea mfano Jumuiya yetu ya Wanawake, Jumuiya ya Vijana umri fulani ukifika unakuwa hauna vigezo, lakini Jumuiya hii haina mipaka hivyo inapaswa kuwa na nguvu kubwa, tutumie ukubwa wa Jumuiya hii kuwasaidia Mwenyekiti wetu na Makamu Mwenyekiti upande wa Zanzibar katika kujenga chama na kuzungumza kwa ukubwa yale yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika," alisema Dk. Biteko.

Dk. Samia na Makamu Mwenyekiti wa CCM kwa upande wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wanataka kuona viongozi wa chama katika ngazi mbalimbali wanawasaidia kazi ikiwamo ya kueleza mafanikio makubwa ya kimaendeleo yanayoendelea kufanyika na kazi kubwa inayofanywa na viongozi hao katika kuwaunganisha Watanzania, kuwa na maridhiano na kujenga uchumi wa nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Dogo Mabrouk, amemshukuru Dk. Biteko kwa kuithamini Jumuiya hiyo na kwa kuiwezesha kwa vitendea kazi ambavyo vitaboresha utendaji kwenye mikoa sita ya Zanzibar na kuahidi kuwa wataendelea kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kabla ya kufanyika kwa kikao hicho, Dk. Biteko alizuru kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume lililopo Kisiwandui.

Aidha, Naibu Waziri Mkuu amekabidhi pikipiki sita kwa ajili ya Jumuiya ya Wazazi (CCM), Zanzibar pamoja kofia ngumu kwa ajili ya jumuiya hiyo kwenye mikoa sita ya Zanzibar.

Alisema, pikipiki hizo ni mali ya Jumuiya ya Wazazi (CCM) na ameelekeza zikafanye kazi ya siasa kama ilivyokusudiwa.

# Namtumbo yapata mwekezaji uzalishaji mbegu bora

**Na Gideon Mwakanosa,**
NAMTUMBO

WILAYA ya Namtumbo mkoani Ruvuma imepata mwekezaji wa kilimo cha mbegu bora za mahindi katika shamba lenye ukubwa wa hekta 1,600.

Mkuu wa wilaya hiyo, Ngollo Malenya amesema serikali pia imelima shamba la mbegu za mahindi na alizeti katika shamba lenye ukubwa wa hekta 2,000.

"Serikali inatarajia kujenga ukuta kwa ajili ya kuboresha ulinzi na mfumo wa umwagiliaji, pia serikali imepanga shamba hilo kuwa sehemu ya utalii wa kilimo hapa nchini," alisisitiza DC Malenya.

Alisema kuwa katika eneo hilo kutakuwa na shule ya kilimo na zitajengwa hosteli za kisasa kwa ajili ya wageni na watalii watakaofika kufanya utalii wa kilimo katika shamba hilo.

Shamba hilo la aina yake nchini, litaongeza wigo wa ajira kwa wazawa na kuongeza mapato yatakayoinua uchumi kwa wananchi na wakala wa mbegu nchini. Katika msimu uliopita Wilaya ya Namtumbo ilizalisha mazao tani 12,500 na msimu huu wilaya inatarajia kuzalisha zaidi ya tani 25,000.

# NHIF yawatoa hofu wanachama huduma kadi zake

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umewatoa hofu wanachama wake kuhusu taarifa ya kusitishiwa huduma, ikisema hakuna kadi za wanachama zilizozuiliwa.

Ufafanuzi huo umetolewa baada ya kuwapo kwa taarifa za kupotosha katika mitandao ya kijamii zikieleza kwamba kadi za wanachama wa mfuko huo zimezuiliwa kupata huduma ama kupata rufani kwenye hospitali za binafsi zilizosajiliwa na NHIF.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Meneja Uhusiano wa NHIF, Grace Michael, iliwataka wanachama wa mfuko huo kupuuzia taarifa hizo ambazo ilisema hazina ukweli wowote.

"Taarifa hizi hazina ukweli wowote na badala yake zina nia ovu ya kuleta taharuki kwa wanachama wa mfuko. Ukweli ni kwamba huduma za matibabu kwa wanachama zinaendelea kama kawaida kupitia vituo zaidi ya 9,000 vilivyosajiliwa vikiwamo binafsi, madhehebu ya dini na serikali," ilieleza taarifa hiyo.

Kadhalika, alieleza kuwa NHIF inawahakikishia wanachama kuwa huduma za matibabu zinaendelea kama kawaida katika vituo vyote vilivyosajiliwa na endapo kutakuwa na mabadiliko taarifa rasmi itatolewa kupitia njia rasmi.

Kadhalika, iliwataka wanachama wa mfuko huo endapo watakutana na changamoto ya kukataliwa huduma katika kituo chochote wanapaswa kutoa taarifa katika ofisi za mfuko zilizo karibu.

NHIF katika taarifa yake juzi ilisema serikali imeunda kamati huru itakayofanya mapitio na kuwasilisha mapendekezo yake serikalini.

Bei mpya zilizotangazwa awali zilipangwa kuanza kutumika Januari Mosi, mwaka huu, lakini kukaibuka sintofahamu baada ya wamiliki wa hospitali binafsi kutishia kusitisha huduma za matibabu kwa wenye kadi za NHIF.

Kadhalika, serikali kupitia Wizara ya Afya, mwishoni mwa wiki ilikutana na watoa huduma kutoka sekta binafsi pamoja na NHIF.

Kikao hicho kililenga kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ya kitita cha mafao kinachotarajiwa kuanza kutumika kwa wanachama wake.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akishiriki upandaji miti kwenye eneo la ofisi ya wilaya hiyo, Kata ya Makulu jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kusiluka ataka watendaji kutembelea wawekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Moses Kusiluka, amewaagiza watendaji wa serikali kujenga mazoea ya kuwatembelea wawekezaji mara kwa mara ili kujua changamoto zao na kuzitatua kwa wakati.

Kadhalika, amepongeza kasi ya ujenzi wa kongani ya viwanda ya SINO TAN inayojengwa eneo la Kwala Kibaha, Mkoa wa Pwani na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuwawekea mazingira rafiki.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea viwanda viwili vya nguo na vipodozi vilivyojengwa ndani ya Kongani hiyo ya SINO TAN.

Kwenye ziara hiyo, Dk. Kusiluka aliambatana na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Viwanda na Biashara na makatibu wakuu wa Wizara ya Uchukuzi, Fedha, Viwanda na Biashara na taasisi mbalimbali.

Alisema watendaji hawapaswi kujifungia kwenye ofisi zao na badala yake wanapaswa kujenga utamaduni wa kuwatembelea mara kwa mara wawekezaji hao ili kujua maendeleo yao na changamoto zao.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji zaidi kutoka nje kwa sera, sheria, vivutio mbalimbali na kuongeza kuwa Tanzania ni eneo salama kwa uwekezaji.

"Kwa muda mfupi tu tumeona namna ambavyo mmeweza kufanya mambo makubwa, tumeona matokeo ya malengo yenu na tunalipa umuhimu wa juu sana suala la kongani hii," alieleza Dk. Kusiluka.

"Kama kuna vitu vya mfano na vya kuonyesha kwa watu huko duniani ni kongani hii kwasababu hatukuwahi kuwa na kitu kama hiki, lakini kwa sasa tunajivuna tuna cha kuwaonyesha wenzetu kwamba na sisi tumeweza kufanya," alisema.

Dk. Kusiluka alimhakikishia mwekezaji serikali itafanya kila linalowezekana mradi huo unakamilika kwa wakati na kuanza uzalishaji kama ilivyopangwa ili kuongeza mauzo ya nje.

Awali, Mratibu wa Kongani ya SINO TAN, Jensen Hung, alisema itakapokamilika wanatarajia kujenga viwanda vya kati na vikubwa 300 na kutoa ajira za moja kwa moja 100,000.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema wizara inatamani kuona kongani hiyo inakamilika kwa wakati na inajaa viwanda vilivyopangwa ili kusaidia kwenye mauzo ya nje na kuongeza ajira.

"Serikali inakila sababu ya kuendelea kumsaidia huyu mwekezaji kwasababu anasaidia ajira kwa vijana wetu na asilimia 90 ya vijana tuliowaona kwenye kiwanda cha nguo wanatoka hapahapa Kibaha," alisema.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu alisema serikali haiwezi kupata kodi mpya bila kuwa na uwekezaji mpya na wizara yake inafurahi kuona idadi ya viwanda nchini inaendelea kuongezeka.

"Ni uhalisia huwezi kuvuna bila kupanda katika uchumi wa kisasa lazima kuwe na sera na sheria nzuri na mazingira rafiki ili kuwavutia wawekezaji wengi wanaouza bidhaa ndani na nje ya nchi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema viwanda vingi vinaendelea kujengwa, lakini vingine vinasuasua kutokana na upungufu wa nishati ya umeme na gesi.

"Katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita Mkoa wa Pwani tumefanikiwa kupata viwanda 30 na saba kati ya hivyo vilikuwa viwanda vidogo, lakini sasa vimekuwa vikubwa hii ni ishara kwamba kuna mazingira mazuri ya uwekezaji," alisema.

# Polisi yaanza kampeni elimu ulinzi shirikishi nyumba za ibada

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi wilayani hapa limeanza kampeni ya nyumba za ibada na mitaani kutoa elimu ya ulinzi shirikishi kwa jamii.

Polisi Kata Wilaya ya Magila, Inspekta Frank Mwemsi, ameanza kampeni hiyo kwa kutoa elimu ya ulinzi shirikishi katika nyumba za ibada misikitini na makanisani.

Akiwa katika Msikiti wa Kata ya Magila juzi, alisema lazima jamii ifahamu faida za ulinzi shirikishi.

Alisema suala la ulinzi sio la polisi pekee ni la wananchi wote kuwafichua wahalifu katika maeneo yao wanayoishi na kutoa taarifa polisi.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwapa watoto mafundisho waliyokuwa wakipewa zamani maadili mema ili kuzuia mmomonyoko wa maadili katika jamii ya Muheza kwa maslahi ya taifa.

Alisema kuwapo vikundi shirikishi katika jamii kutasaidia kupunguza vitendo vya uhalifu ikiwamo uporaji, wizi na udhalilishaji.

Imamu wa msikiti huo, Kassim Makame amelishukuru Jeshi la Polisi kwa kuwapatia elimu ya ulinzi shirikishi katika msikiti huo.

Katika hatua nyingine alimwomba polisi kata kuwatafutia wafadhili wa kuwapa msaada wa mabusati ya kutandika ndani ya msikiti, kuweka dari na kuwajengea madrasa ili watoto wasome elimu ya dini.

Mwalimu wa madrasa katika msikiti huo, Ramadhan Hassan Omari, alisema elimu ya ulinzi shirikishi waliopewa wataifanyia kazi.

# Katambi aagiza OSBP kudhibiti usafirishaji watoto njia za panya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, ameagiza Kituo cha Huduma za Pamoja katika mpaka wa Namanga (OSBP), kuboresha ukaguzi ili kudhibiti usafirishaji watoto na watu wenye ulemavu kwa njia ya panya.

Alisema kuna baadhi ya malori na mabasi ya abiria yamekuwa yakitumika kusafirisha makundi hayo ya watu kwenda nchini Kenya kwa njia isiyo ya halali hivyo waongeze kasi ya utoaji huduma ili kumaliza tatizo hilo. Katambi alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki akiwa mkoani Arusha, baada ya kukagua utoaji huduma katika mpaka huo unaozitenganisha nchi za Tanzania na Kenya ikiwa ni lengo la serikali kukuza ufanisi ili kuondoa kero kwa wasafiri.

Alisisitiza watoa huduma hao kusimamia suala la ulipwaji wa kodi ili serikali ipate mapato kwa ajili ya kuwezesha kudhibiti watu wenye nia ovu, ambao hutumia watoto na watu wenye ulemavu kuwapitisha maeneo ya mipakani. "Nataka huduma za pamoja mziimarishe zaidi, ikiwamo kubaini watu wanaosafirisha binadamu unaofanyika maeneo ya mipakani ikiwamo wale wanaotumia fursa za kusafirisha watoto na watu wenye ulemavu kwenda nchi nyingine kuwatumikisha.

"Serikali imewekeza fedha nyingi katika kituo hiki na vifaa vya kisasa, vimewekwa turahisishe utoaji huduma ikiwamo kaguzi zaidi kwenye malori, mabasi na abiria lakini dhibitini wanaotumia njia za panya kusafirisha makundi haya,"alisema.

Alisema Rais Samia Hassan ameweka mfumo mzuri wa watu kupata hati za kusafiria, hivyo ni lazima wazingatie sheria katika kupata hati hizo, ili wafanye biashara zao kwa halali, katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Aidha, aliwaagiza wataalamu kuzingatia hali ya usalama katika mipaka kwa kufanya upekuzi wa abiria na mizigo yao pamoja na magari ya mizigo kwa umakini na kujiridhisha.

Aliwakumbusha kuhakikisha raia wanaovuka mpaka huo wanavyo vibali vyote halali, ili kuzuia uhamiaji haramu na upitishaji wa bidhaa za magendo.

Pia alisisitiza urahisishwaji wa mizigo na kaguzi mipakani zifanyike kwa haraka, ikiwamo udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza yasiweze kuenea kwa binadamu na mifugo.

Ofisa Mfawidhi wa kituo hicho, Gulugu Nkanga, alimweleza Naibu Waziri huyo kwamba, sheria ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki inayoruhusu raia wa mpakani wa nchi zote mbili, kuvuka mpaka bila kuwa na hati za kusafiria ndani ya kipenyo cha kilomita 20 imeleta mafanikio kibiashara .

"Kupitia ruhusa hii wananchi hufanya biashara na maeneo mengi ya Tanzania watu wake huja nchini, kwa kutumika kilomita hizo kwa ajili ya kutembea na kunywa vinywaji kisha kurudi nchini kwao, bila kubughudhiwa na maofisa uhamiaji wa nchi zote mbili yaani Kenya na Tanzania.

Wakati huo huo, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marko Ng'umbi, alisisitiza hali mpaka huo ipo salama na kuongeza kuwa serikali inaboresha huduma za utoaji hati za kusafiria sanjari na kaguzi ikiwemo uimarishaji wa ulinzi na usalama.

# Wanaokata mikoko kuchukuliwa hatua

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI mkoani Tanga, imesisitiza kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kujihusisha na ukataji miti ya mikoko kwa sababu kufanya hivyo ni kuharibu mazingira ya ikolojia hiyo.

Wanaotajwa kuharibu rasilimali hizo za bahari ni wale wanaojihusisha na shughuli za baharini wakiwamo wavuvi, wavunaji chumvi na wajenzi wa kambi.

Mkuu wa Mkoa huo, Waziri Kindamba, aliyasema hayo juzi na kusisitiza kuwa serikali kamwe haitofumbia macho suala hilo na yeyote atakayebainisha atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za mazingira.

"Kwa hili, tunatoa tahadhari jamii kuwa mstari wa mbele kushiriki katika utunzaji wa mazingira, kwa sababu ya umuhimu wake mkubwa taifa.

Alisema katika kuhakikisha kuwa miti hiyo inahifadhiwa serikali ilifanya warsha ya ushirikishwaji viongozi wa serikali kuhusu utekelezaji wa mradi wa uhifadhi ya mikoko kwenye ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Alisema kwa sasa kinachoendelea ni vita endelevu dhidi ya wale wanaotaka kuiharibu rasilimali hiyo na kinga kuu dhidi ya ikolojia ya bahari.

Aidha, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema uhifadhi wa mazingira umeelezwa kwa namna tofauti katika Biblia Takatifu na Quran tukufu, hivyo jitihada zinazoendelea hivi sasa ni sehemu yaliyomo kwenye vitabu hivyo.

Alisema kwamba mikoko ina faida nyingi kwa mazingira na binadamu ikiwemo kuzuia mmomonyoko wa ardhi kwenye kingo za bahari, kutengeneza asali iliyo bora, chakula, mazalia ya samaki, nishati na ujenzi.

Ofisa Elimu Mazingira wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Martha Ngalowera, alisema utoaji wa mafunzo ikiwemo ya uhifadhi wa mazingira, ni muhimu kwa viongozi wa Serikali kwa vile wanashiriki katika kutunga na kusimamia miongozo, mikakati na kanuni za uhifadhi wa mazingira nchini.



Mbunge wa Viti Maalum wa Vyuo Vikuu, Dk. Pauline Nahato (kulia), akimtibu mmoja wa wagonjwa waliokumbwa na maafa ya maporomoko ya matope Mlima Hanang' kwenye Hospitali ya Wilaya ya Hanang' (Tumaini) hivi karibuni. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kamati ya Amani Hanang' kuwaombea waliopoteza maisha mafuriko ya tope

**Na Allan Isack,** HANANG'

KAMATI ya Amani ya Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara, kwa kushirikiana na ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo, wameandaa maombi maalum kwa ajili ya waliopoteza maisha katika maafa aliyotokea Desemba 3 mwaka jana.

Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, katika maafa hayo yaliyotokana na maporomoko ya tope, mawe na magogo kutoka katika mlima Hanang watu 89 walipoteza maisha na wengine 139 kujeruhiwa vibaya.

Maombi hayo yanayolenga ya kuomba rehema za Mwenyezi Mungu na kuhusisha viongozi na waumini wa madhehebu mbalimbali, yanatarajiwa kufanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Katesh.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja, alithibitisha kufanyika kwa tukio hilo litakaloongozwa na kamati ya amani ya wilaya hiyo.

Mmoja wa wakazi wa Mji mdogo wa Katesh, Morris Assey, alipongeza kamati hiyo kwa kuandaa maombi ya kuwakumbuka waliotangulia mbele za haki kwa kushirikiana na ofisi ya mkuu wa Wilaya.

"Hakika tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu na kuwaombea wenzetu waliotangulia mbele za haki, asanteni viongozi wanaozidi kutuongoza katika kipindi chote cha wakati mgumu kwa Hanang'," amesema.

Mkazi mwingine, Hamis Ally, alisema kitendo cha viongozi kuandaa dua na salama kwa ajili ya maombi ya pamoja kwa madhehebu tofauti ni cha kuungwa mkono.


"Viongozi wa kamati ya amani na Mkuu wa Wilaya ya Hanang' Janeth Mayanja wanastahili pongezi kwa kuandaa maombi haya kwa ajili ya ndugu zetu," alisema.





# Wazazi wasiopeleka watoto shule wanyooshewa kidole

**Na Waandishi Wetu**



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, akizungumza katika mkutano wa hadhara alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa sekondari mpya ya Kijiji cha Wanyere, Wilaya ya Musoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WAKURUGENZI wa halmashauri wameahidi kuwachukulia hatua za kisheria wazazi na walezi wote watakaoshindwa kuwapeleka shule wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza pamoja na wale wanatakiwa kuanza masomo ya awali kwa mujibu wa sheria.

Hatua hiyo inakuja wakati shule nchini zikianza kufunguliwa leo huku baadhi ya walezi na wazazi wakilalamikia kupaa kwa bei za bidhaa za shule hali inayowafanya washindwe kuzimudu.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Hellen Rocky, aliiambia Nipashe kuwa maandalizi ya kupokea wanafunzi yamekamilika hivyo ni wajibu wa kila mzazi au mlezi kupeleka watoto shule bila kujali hali walizonazo.

Aliwasihi wazazi kuhakikisha wanafunzi hao wanaripoti kwa muda uliopangwa katika vituo husika na kuwahakikishia kuwa watoto wanaenda kupata elimu bora kwani tayari mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wanapata ufaulu mzuri imeshawekwa.

Aidha, alitoa onyo kwa wale wazazi ambao watoto wao hawataripoti shuleni kuwa uchunguzi utafanyika kwa wanafunzi hao na hatua kali zitachukuliwa.

Alisema tayari miundombinu ipo ya kumudu idadi ya wanafunzi walopangwa katika shule husika huku akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha ujenzi wa madarasa kwa shule za sekondari pamoja na msingi hivyo kuahidi wanafunzi wote kupokelewa vizuri.

Kuhusu usajili wanafunzi wa awali na darasa la kwanza alisema unaendelea vyema na mpaka sasa wanafunzi wa awali wamefikia asilimia 54.3, darasa la kwanza asilimia 79.1 na asilimia 37 kwa Memkwa.

"Tumejipanga kuhakikisha hakuna mtoto anaesitahili kwenda shule atabaki mtaani na wanafunzi hawa wote watakaoendelea kujiandikisha watapokelewa vizuri kwani miundombinu ni mizuri, walimu wapo pamoja na vifaa vya kujifunzia,"alisema Rocky.

Kaimu Mkurungezi wa Manispaa ya Shinyanga, Mhandisi Kassimu Thadeo, aliwataka wazazi kutokuwa na visingizio katika suala la kuwapeleka watoto shule kwani serikali haitakuwa tayari kuvisikiliza.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwapeleka shule watoto wote ambao wameshafikisha umri wa kuanza masomo, pamoja na wale ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ili wapate elimu na kutimiza ndoto zao.

"Mtoto ambaye hatakuwa na sare za shule mzazi asisite kumpeleka shule kuanza masomo, ampeleke wakati akiendelea kujipanga kumnunulia sare hizo ili asikose masomo,"alisema Mhandisi Thadeo.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza, Hassan Masala, alipiga 'stop' utaratibu wa wakuu wa shule na wakurugenzi kuorodhesha viti na meza katika fomu za kujiunga na shule kama sehemu ya mahitaji ya kujinga na shule wilayani humo.

Alisema kama wilaya wamefanya juhudi za kuhakikisha shule zinapata madawati hivyo hilo siyo suala la kuwazuia watoto kuanza shule na halitakiwe kuwapo kabisa kwenye mahitaji yake.

"Vilevile kwa wale wanaowalazimisha wazazi kupeleka rimu tatu katika shule nao hatutawavumilia kwani haiwezekani kila mwanafunzi atumwe rimu zote hizo kama hakuna mahitaji mengine ya ziada," alisema DC Masala.

Aliwaelekeza viongozi wa elimu msingi na sekondari kuhakikisha wanakagua fomu za kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kuangalia ni mahitaji yapi ya msingi yanayotakiwa kubaki katika fomu hizo mengine yaondolewe ili kuondoa vikwazo kwa wanafunzi kuripoti shule.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Wilabuzu Ludigija, alitoa onyo kwa wazazi wote watakaokaidi maagizo ya kuwapeleka wanafunzi shule na kuwaacha wanaendelea na shughuli za kuchunga mifugo na kulima kuwa wote watachukuliwa hatua za kisheria.

"Jumatatu (leo) mimi pamoja na Mkurugenzi tumepanga kutembea kila shule kujihakikishia kuwa watoto wote wameenda kuandikishwa kuanza shule na kujiunga na kidato cha kwanza maana miundombinu imetengenezwa kwa ajili yao," alisema Ludigija.

**VILIO VYATAWALA MAHITAJI YA SHULE KUPANDA BEI**

Wakati wito huo ukitolewa, wazazi na walezi katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya kanda ya ziwa wamelalamikia tabia za baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa za shule hususani katika kipindi hiki wanapoanza masomo.

Frola Mtabuzi Mkazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera alitaja bidhaa zilizopanda bei kuwa ni pamoja na sare za shule, viatu, mabegi pamoja na madaftari tofauti na vilivyokuwa vikiuzwa awali alitaja hali hiyo kukwamisha shughuli za maendeleo ya watoto wake.

Mzazi Mwingine Jesca Jason alitaja kupanda kwa bidhaa hizo muhimu kwa kipindi hiki kuwa moja ya sababu ya wanafunzi kuchelewa kuanza shule huku akiiomba serikali kuingilia kati ya mfumuko huo usiyo rasmi.

Mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, Luhende Natujwa, aliomba serikali kutoa tamko juu ya bidhaa hizo kuendelea kupaa na kutaja hali ya kipato cha wananchi kutofautiana hatua aliyoitaja kusababisha wengine kushindwa kutimiza mahitaji ya watoto wao licha ya elimu kuwa bure.

**WAFANYABIASHARA WANENA**

Wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali kanda ya ziwa wameonesha kutofautiana katika kauli wakitaja gharama za maisha kupaa kuwa chanzo cha bidhaa kupanda pia huku wengine wakitaja baadhi hizo kuwa hazijapanda bali ni hofu ya wazazi kutokana na matumizi makubwa waliyokuwa nayo wakati wa sikukuu.

Mfanyabiashara kutoka Manispaa ya Bukoba, Deo Assey, alisema "bei za mahitaji ya shule ni zile zile japo wateja wanaonekana kulalamika kutokana na hali ya ugumu wa maisha pamoja na matumizi ya makubwa ya hela kipindi cha sikukuu kupelekea wazazi kukosa pesa za kufanya maandalizi ya shule kwa watoto wao".

Mfanyabiashara wa vifaa vya shule mkoani Shinyanga Amina Juma, alikiri bidhaa hizo kupanda bei na kusema kuwa daftari linauzwa Sh.800 kutoka Sh.700, huku kaunta book zikiuzwa Sh. 2,500 kutoka 2,000 kulingana na ukubwa na zingine zikiuzwa Sh. 3,500 kutoka 3,000 na kutaja hali hiyo kutokana na kupanda kwa gharama za usafirishaji.

Morisi Mraonde Mfanyabiashara wa viatu vya wanafumzi Mtaa wa Serengeti mkoani Mara, alitaja kubanda kwa nauli pamoja na bei za kulangua kuwa sababu bidhaa hizo kuwa juu mtaani.

Alisema kiatu kilichokuwa kinauzwa Sh.10,000 kwa sasa kinauzwa kwa Sh.20,000 sawa na tofauti ya Sh.10,000 na kuwataka wazazi kuvumilia hali hiyo kwa siyo makusudi yao kufanya hivyo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika Soko la Mlango Mmoja jijini Mwanza, Jackson Anthony, aliwataka wafanyabiashara katika soko hilo kuacha tabia ya kupandisha bidhaa bila utaratibu maalum uliowekwa kwani kufanya hivyo ni kinyume na utaratibu.

Naye Diwani Kata Turwa, Chacha Marwa Machugu, aliwataka wafanyabiashara kuepuka kupandisha bei vifaa vya shule ili kuwapunguzia wazazi gharama za manunuzi ya vifaa ili wanafunzi waende shule.

Musukuma alisema halmashauri hiyo chini ya ushirikiano wa Mwenyekiti, Daniel Komote, Mkurugenzi, Gimbana Ntovya, pamoja na Mbunge wa Jimbo la Tarime Michael Kembaki, wamejipanga vyema kuhakikisha hakuna mzazi ambaye ataombwa kuchangia kununua kiti na meza kwa ajili ya kupeleka shule.

**Imeandaliwa na Jenesta Jasson (KAGERA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Timoth Itembe (MARA), Thomas Wandiba (SAUT), Vitus Audax (MWANZA).**

Nipashe
Spotika



USAJILI BORA WA JANUARI 'BIG SIX' EPL 12 - 13




# MAMBO MA5 USIYOYAJUA KUHUSU MARTIN ODEGAARD

**LONDON, Eangland**

MARTIN Odegaard ni mmoja wa wachezaji bora Arsenal na ni nahodha wa Norway, kwa hivyo hapa kuna kila kitu unachohitaji kujua kuhusu kiungo huyo anayeongoza klabu na nchi yake.

Mchezaji huyo amekuwa kwenye Uwanja wa Emirates tangu Januari 2021 baada ya Arsenal kumsajili kwa mkopo kutoka Real Madrid. Juhudi zake katika nusu ya mwisho ya msimu huo zilimshawishi kocha Mikel Arteta kurejea 'Los Blancos' mwezi Agosti na kukubali uhamisho wa kudumu wa pauni milioni 34.

Kufanya kazi chini ya Arteta kaskazini mwa London kumemwona Odegaard akiendelea kupiga urefu mpya katika uwezo wake. Odegaard pia alichukua nafasi ya Pierre-Emerick Aubameyang kama nahodha wa kikosi cha kwanza cha Arsenal mnamo Julai 2022. Alichukua jukumu hilo kwa kudumu kama nyongeza ya Arteta ambaye anaweka viwango.

Odegaard alikuwa amekaa Real Madrid kwa miaka sita kabla ya kuondoka 'Galacticos' na kwenda Arsenal. Los Blancos walilipa Stromsgodset pauni milioni 2.5 kumsajili mchezaji huyo akiwa na umri wa miaka 16 Januari 2015. Lakini baada ya uhamisho wa mkopo, alicheza mara 11 pekee katika timu ya Santiago Bernabeu.

Real Madrid ilimtoa kwa mkopo Odegaard kwa Heerenveen, Vitesse Arnhem na Real Sociedad kabla ya kuhamia Arsenal mwaka wa 2021.

Lakini Odegaard ni nani? Hapa kuna kila kitu unachohitaji kujua juu yake...

**Umri wake**

Odegaard ana umri wa miaka 24. Kiungo huyo alizaliwa mnamo Desemba 17, 1998 na alianza kazi yake na akademi ya Drammen Strong mnamo 2005.

**Martin Odegaard alizaliwa wapi?**

Martin Odegaard alizaliwa huko Drammen, jiji lililoko mashariki mwa Norway takriban maili 27 kusini-magharibi mwa Oslo. Pia ni jiji la sita kwa ukubwa nchini Norway lenye wakazi 100,000.

**Mpenzi wake**

Odegaard inaonekana alimthibitisha Helene Spilling kuwa mpenzi wake mnamo Juni 2023. Nyota huyo wa Norway alitoa mkusanyiko wa picha za pamoja kwenye Instagram baada ya wawili hao kuonekana wakihudhuria tuzo za soka za London wakiwa pamoja Machi mwaka huo.

Odegaard pia alijumuisha picha za Spilling akihudhuria mechi za Arsenal kwenye Uwanja wa Emirates kumuunga mkono. Spilling ni mcheza dansi wa Norway na muigizaji kwenye televisheni. Alizaliwa katika Manispaa ya Gjerdrum nchini Norway mnamo Aprili 17, mwaka 1996.

**Gari analoendesha**

Odegaard anamiliki gari aina ya Audi RSQ3 na mara nyingi amekuwa akizongwa na mashabiki wa Arsenal wakati akirudi nyumbani kutoka Uwanja wa Emirates. Gari la matumizi ya michezo lina injini ya petroli ya silinda tano na bei inayopendekezwa ya rejareja linaponunuliwa jipya ni kati ya pauni 55,000 hadi 65,000.

**Ndugu wa Odegaard**

Odegaard anatoka katika familia ya watu sita huku kiungo huyo akijivunia ndugu zake watatu. Ana dada wawili, Mari na Emile, na kaka mmoja, Kristoffer. Wazazi wa Odegaard ni baba, kiungo wa zamani wa Norway na Stromsgodset, Hans Erik, na mama, Lene Cecilie.

Familia ya Odegaard mara nyingi ni watu wa wenye ubinafsi ambao hawapendi kujulikana. Baba yake, Hans Erik, ameendelea kujihusisha na soka tangu alipostaafu kama mchezaji mwaka wa 2007. Alicheza kwa miaka 14 kati ya vipindi vya Stromsgodset na Sandefjord kabla ya kuwa kocha mwaka 2009.

Hans Erik alifanya kazi kwa muda mfupi kama kocha wa timu ya Real Madrid ya Chini ya 17 kutoka 2015 hadi 2017.

Lakini baadaye alirejea Mjondalen kufundisha kikosi cha vijana hadi 2018. Mtaalamu huyo pia alichukua jukumu la kuinoa timu yake ya zamani, Sandefjord, mnamo 2021.

## ISIKUPITE

LICHA ya Arsenal kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya West Ham Desemba 28, mwaka jana, ilivunja rekodi ya Ligi Kuu ya England kwa kuguswa mpira mara nyingi zaidi ndani ya eneo la hatari la wapinzani bila kufunga bao. Arsenal ilimiliki mchezo kwa asilimia 75 na kupiga mashuti 30 na manane yakilenga goli, hawakuweza kupata njia ya kumpita Alphonse Areola. 'The Gunners' waligusa miguso 77 ndani ya eneo la hatari la West Ham, ikiwa ni idadi ya juu zaidi iliyorekodiwa huku timu ikishindwa kufunga tangu rekodi za Opta zilipoanza mwaka 2008.



# USAJILI BORA WA JANUARI 'BIG SIX' EPL



VIRGIL VAN DIJK

**LONDON, England**

DIRISHA la uhamisho la Januari linaweza kuhisi kana kwamba limekuwa likipangwa katika Kalenda ya Ligi Kuu England, lakini kwa hakika lilianza kutumika msimu wa 2002-03.

Kabla ya mfumo wa usajili wa madirisha mawili kama tunavyoujua leo, klabu za Ligi Kuu England ziliruhusiwa kufanya biashara ya wachezaji katika msimu mzima hadi Machi 31.

Mfumo wa madirisha mawili ulibuniwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kama njia ya kuwazuia wachezaji kutoka kwenye klabu watakavyo, huku wakiwaruhusu kuuzwa katika muda uliowekwa - yaani, madirisha ya majira ya joto na majira ya baridi.

Arsenal, Chelsea, Liverpool, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur zote zimekumbana na bahati tofauti linapokuja suala la soko la msimu wa baridi.

Timu hizo sita kubwa za Ligi Kuu England zimekamilisha usajili wa takribani wachezaji 200 kwa vikosi vyao vya kikosi cha kwanza wakati wa Januari tangu mwaka 2003.

Chelsea na Tottenham ndizo zilizoshiriki zaidi wakati huo, na kusajili wachezaji 39 na 40. Wakati Manchester United - labda kwa kushangaza - wamefanya biashara ndogo zaidi wa wachezaji 22.

Kwa pamoja timu hizo sita zimetumia zaidi ya pauni bilioni 1.83 katika dirisha la majira ya baridi hadi sasa, huku Chelsea wakiwa ndio watumiaji wakubwa zaidi kwa kiasi kikubwa cha fedha (pauni milioni 628.94) na Manchester United ndiyo iliyotumia fedha nyingi zaidi kwa jumla (pauni milioni 179.65). Chelsea pia imesajili wachezaji wengi zaidi katika dirisha moja la majira ya baridi, baada ya kuleta wachezaji nane wapya (kwa ada ya jumla ya pauni milioni 296.7) Januari 2023.

Tumechunguza kila uhamisho wa kikosi cha kwanza unaoingia (pamoja na mikataba yote ya kudumu, mikopo na uhamisho wa bila malipo) uliofanywa Januari na kila klabu kubwa zaidi ya Ligi Kuu England katika miongo miwili iliyopita na tukachagua usajili bora zaidi uliofanywa Januari.

**Arsenal**

**1. Martin Ødegaard (aliyesajiliwa kutoka Real Madrid, kwa mkopo), Januari 27, 2021**

Baada ya kujiunga na Real Madrid kama kinda mwenye umri wa miaka 16, mwaka 2015 na kupata mechi chache kati ya mfululizo wa mkopo, Ødegaard alihamia Arsenal kwa miezi sita kutafuta mwanzo mpya akiwa na umri wa miaka 22. Kiungo huyo wa kati wa Norway alikuwa mchezaji bora wa papo kwa papo na hivi karibuni alirejesha ari yake ya ubunifu, haraka akaingia kwenye safu ya kiungo ya 'Washikabunduki' kabla ya kufanya uhamisho wake kuwa wa kudumu kwa takribani pauni milioni 40 msimu wa majira ya joto. Sasa ni nahodha wa klabu, hiyo ni sawa na kusema usajili uliofanikiwa zaidi.

**2. Theo Walcott (Southampton, pauni milioni 5), Januari 20, 2006**

Akiwa amesajiliwa na Arsene Wenger miezi sita tu baada ya kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha Southampton kama winga mahiri, mwenye umri wa miaka 16, Walcott alitumia miaka 12 na nusu ya maisha yake ya uchezaji akiwa Arsenal, akifunga mabao 108 katika mechi 400 na kushinda mataji matatu ya FA.

**3. Pierre-Emerick Aubameyang (Borussia Dortmund, pauni milioni 56), Januari 31, 2018**

Mchezaji aliyesajiliwa kwa rekodi ya klabu wakati huo, Aubameyang alilipa imani kwa kufunga mabao 10 katika michezo 13 katika kipindi chake cha kwanza cha nusu msimu. Mshambuliaji huyo kisha akashiriki Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England katika kampeni yake ya kwanza kamili (2018-19) kabla ya kuwa nahodha wa kikosi hicho kilichoshinda fainali ya Kombe la FA 2019-20, akifunga mara mbili dhidi ya Chelsea.

Hatimaye aliondoka Februari 2022 baada ya masuala ya kinidhamu kuharibu uhusiano wake na kocha Mikel Arteta, lakini angalau alifan- ya hivyo baada ya kufunga mabao 92 ya kuvutia katika michezo 163 kwa klabu hiyo.

**Chelsea**

**4. Olivier Giroud (Arsenal, pauni milioni 18), Januari 31, 2018**

Giroud aliwasili kutoka kwa wapinzani wa Chelsea Arsenal kwa mkataba wa awali wa miezi 18 akiwa na umri wa miaka 31. Huku akikataliwa na wengi kama nyongeza ya chini kwenye kikosi, mkongwe huyo alichangia pia ushindi wa Chelsea wa Ulaya msimu wa 2018-19 (alimaliza kama mfungaji bora wa mashindano akiwa na mabao 11, likiwamo moja dhidi ya klabu yake ya zamani ya Arsenal kwenye fainali) na pia alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA wakati wa miaka mitatu na nusu ya kukaa Stamford Bridge.

**2. Branislav Ivanovic (Lokomotiv Moscow, pauni milioni 9.7) Januari 16, 2008**

Jina lisilojulikana alipowasili, Ivanovic alionekana haraka kuwa safu ya ulinzi ya Chelsea chini ya makocha kadhaa tofauti. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Serbia, alikaa kwa misimu 10 Stamford Bridge, akicheza michezo 377 na kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu, matatu ya Kombe ya FA, Kombe la Ligi, Ligi ya Europa na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**3. Nemanja Matic (Benfica, pauni milioni 21) Januari 15, 2014**

Matic alirejea Chelsea katika dirisha la Januari 2014 baada ya kuondoka kwa mara ya kwanza katika klabu hiyo kama sehemu ya mkataba ambao ulimfanya David Luiz kuwasili Stamford Bridge kutoka Benfica miaka mitatu iliyopita. Kiungo huyo wa kati wa safu ya ulinzi wa Serbia alipoteza muda kidogo chini ya Jose Mourinho na alicheza zaidi ya mara 150 katika misimu mitatu na nusu iliyofuata huku akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu England, Kombe la FA na Kombe la Ligi. Kisha akajiunga na Manchester United kwa ada yenye thamani ya karibu mara mbili ya Chelsea iliyolipa.

**LIVERPOOL**

**1. Luis Suarez (Ajax, pauni milioni 22.7) Januari 31, 2011**

Suarez akiwa mchezaji bora zaidi wa usajili wa Januari kwenye rekodi, alianza vema na kuendelea kuimarika zaidi kwa Liverpool, huku mavuno yake yakiongezeka kwa mwaka wakati mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay alipoondoka kwenda Barcelona akiwa na mabao 31 katika mechi 33 za Ligi Kuu England. Hesabu hiyo ilitosha kumshindia tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Kuu, pia Kiatu cha Dhahabu na Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya, miongoni mwa sifa nyinginezo zake binafsi.

**2. Virgil van Dijk (Southampton, pauni milioni 75), Januari 1, 2018**

Huenda aligharimu fedha nyingi lakini Liverpool hawakusajili tu beki wa kati maridadi, wa kiwango cha kimataifa, bali pia mchezaji bora wa ulinzi wa timu ya Jurgen Klopp. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi bado yuko katikati ya safu ya beki ya Klopp akiwa na umri wa miaka 32, sasa anaongoza timu ambayo imeshinda mataji sita makubwa ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu -- tangu kuwasili kwake.

**3. Philippe Coutinho (Inter Milan, pauni 8.5), Januari 30, 2013**

Coutinho alipiga kiwango bora zaidi cha maisha yake yote ndani ya Liverpool, akichangia safu nzuri zaidi ya ushambuliaji pamoja na Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino. Mshambuliaji huyo wa Kimataifa wa Brazil, alikaa Anfield kwa misimu mitano na nusu bila kushinda kombe lolote lakini alifunga mabao 54 na asisti 45 katika mechi 201 kabla ya kuondoka kwenda Barcelona kwa uhamisho wa pauni milioni 120. Ni sawa kusema fowadi huyo, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Al-Duhail kutoka Aston Villa, amekuwa hana tena ubora ule kwa muda mrefu tangu aondoke Anfield.

**Manchester City**

**1. Edin Dzeko (Wolfsburg, pauni milioni 27), Januari 7, 2011**

Hapo awali Dzeko alikuwa amefunga mabao 66 katika michezo 111 akiwa na Wolfsburg na kusaidia klabu hiyo kunyakua taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu wa 2008-09. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Bosnia na Herzegovina kisha akawa mchezaji wa tisa kusajiliwa na Roberto Mancini pale City na aliendelea kuimarika akifunga mara 72 katika michezo 189 na kucheza sehemu yake katika ushindi wa mataji mawili ya Ligi Kuu - ikiwa ni pamoja na ushindi wa kihistoria wa City msimu wa 2011-12.

2. Gabriel Jesus (Palmeiras, pauni milioni 27), Januari 19, 2017

Baada ya City kupata dili la kumnunua Gabriel Jesus mnamo Agosti 2016, ilikubaliwa na pande zote kwamba fowadi huyo wa Brazil akiwa na umri wa miaka 19 angesalia Palmeiras kwa miezi sita kabla ya kuhamia City Januari 2017. Fowadi huyo mahiri alikaa miaka mitano na nusu hapo Etihad ambapo mara kwa mara alijikuta akitumika kama msaidizi wa Sergio Aguero. Bado, alifunga mabao 95 katika mechi 236 na kushinda mataji nane makubwa akiwa na City kabla ya kusajiliwa na Arsenal kwa pauni milioni 45 majira ya joto 2022.

**3. Julian Alvarez (River Plate, pauni milioni 14.1), Januari 31, 2022**

Mmoja wa vijana waliotamaniwa sana na vipaji vya ushambuliaji nchini Argentina, City awali ilikubali kumruhusu Alvarez kubaki River Plate kwa mkopo hadi majira ya joto 2022. Alipotua City kwa mara ya kwanza, alikaimu nafasi kadhaa za juu kabla ya kujiweka kikosi cha kwanza na kutwaa Kombe la Dunia la 2022 na mataji matatu ndani ya miezi saba.

**Manchester United**

**1. Nemanja Vidic (Spartak Moscow, pauni milioni 7), Januari 5, 2006**

Baada ya kuonesha kiwango kizuri katika Ligi ya Urusi, United walilazimika kuzuia ushindani kutoka kwa klabu pinzani kote barani Ulaya kumsajili Vidic Januari 2006. Beki huyo wa kati wa Serbia alikuja kutambulika kwa haraka sana Old Trafford na akawa nahodha wa klabu mwaka wa 2010. Bila shaka ni mmoja wa walinzi bora, na wagumu zaidi kuwahi kucheza kwenye Ligi Kuu.

**2. Patrice Evra (Monaco, pauni milioni 5.5), Januari 10, 2006**

Akiwa amesajiliwa siku tano baada ya Vidic, Evra vile vile alikua mlinzi kwenye safu yenye mafanikio makubwa chini ya Sir Alex Ferguson kati ya miaka ya 2000 na mwanzoni mwa 2010, akishinda mataji matano ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati huo. Beki huyo wa kushoto wa Ufaransa alicheza mechi 379 akiwa na 'Mashetani Wekundu' kabla ya kuondoka kwenda Juventus msimu wa 2014-15.

**3. Bruno Fernandes (Sporting Lisbon, pauni milioni 46.6), Januari 30, 2020**

Akiwaingiza wapendwa wa Louis Saha na Juan Mata kwenye orodha hii, Fernandes amekuwa mmoja wapo wa nuru chache katika historia ya hivi majuzi ya United. Kiungo huyo wa kati wa Ureno amefunga mabao 69 na kutoa pasi za mabao 59 katika michezo 208 tangu ahamie kutoka Sporting CP zaidi ya miaka mitatu na nusu iliyopita akichangia mabao mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote wa United ambaye amekusanya katika kipindi hicho.

**Tottenham**

**1. Jermaine Defoe (West Ham, pauni milioni 7), Februari 4, 2004; (Portsmouth, pauni milioni 9), Januari 6, 2009**

Mchezaji pekee katika historia ya Ligi Kuu kusajiliwa na klabu moja mara mbili katika dirisha la Januari, Defoe alitambulishwa na Spurs mara mbili akiwa na msimu mmoja tu akiwa Portsmouth na kuhesabu mara mbili mafanikio yake huko White Hart Lane - katika kipindi hicho, ambapo alifunga jumla ya mabao 140 katika michezo 361.

**2. Dele Alli (MK Dons, pauni milioni 5), Februari 2, 2015**

Hapo awali Alli alisaini Tottenham dakika 10 tu kabla ya tarehe ya mwisho ya Januari 2014-15, kukiwa na mpango wa kuweka kiungo huyo mwenye kipaji akiwa na umri wa miaka 18, alitua kwa mkopo katika Klabu ya MK Dons kwa muda uliosalia wa msimu. Alipata mafanikio ya papo hapo huko Spurs chini ya Mauricio Pochettino, akichanua na kuwa nguvu ya ubunifu katika misimu michache iliyofuata kabla ya kupoteza sana kiwango, utimamu wa mwili na ari chini ya kocha mpya, Jose Mourinho.

**2. Lucas Moura (PSG, pauni milioni 25), Januari 31, 2018**


Baada ya kugombana na PSG na kujikuta akikaa benchi, Tottenham walipata nafasi ya kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mwanzoni mwaka 2018. Ingawa kiwango cha Moura hakikuwa kizuri sana baadaye.

## Nukuu

"Kiwango cha mchezaji anayehitajika Arsenal kwa sasa ni mtu ambaye anakimbia chini, mshambuliaji wa mwisho, kama [Victor] Osimhen wa dunia hii ... kiwango hicho cha mshambuliaji. Ikiwa Arsenal wanataka kufanya hivyo sasa watahitaji kiwango hicho mfungaji ambaye ataingia moja kwa moja. Hicho ndicho wanachohitaji sasa. Sidhani kama shabiki yeyote wa Arsenal ataangalia mchezo na asione kwamba tunahitaji muuaji mbele ya lango," **Ian Wright akitaja mchezaji wa 'kiwango cha juu' anayepaswa kusajiliwa Arsenal ili kuwa kwenye mbio za ubingwa.**



"Kucheza na Leo Messi hakika ni kitu ninachokikosa sana. Siku zote hukosa kutocheza na Leo Messi tena! Kwa mshambuliaji kama mimi, ambaye napenda kushambulia nafasi, ukiwa naye, una uhakika kwamba unaweza kupata mpira. Ilikuwa anasa ambayo karibu tu ndiye anayeweza kukupa! Zaidi ya hayo, kucheza na Messi ilikuwa ya kipekee!" **Nyota wa PSG, Kylian Mbappe, akikiri kukosa kucheza pamoja na Lionel Messi aliyetimkia Inter Miami ya Marekani.**



"Katika wakati wangu, ilikuwa ni timu mbili (Arsenal na Manchester United) ambazo zingeweza kushinda na kisha Chelsea wakaja. Sasa ukiitazama, Liverpool wamo ndani, [Aston] Villa wamo, ingawa hakuna aliyetarajia wangekuwamo," **Gwiji wa Arsenal, Thierry Henry, akieleza kwa nini ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu utakuwa 'mgumu zaidi kushinda'.**





KICHUYA

# WACHEZAJI 8 WAZAWA MBIONI KUHAMA KATIKA DIRISHA HILI

**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka ya hivi karibuni mashabiki wa soka nchini wamekuwa wakifurahishwa au kuridhishwa zaidi na usajili wa wachezaji kutoka nje ya nchi.

Pamoja na hayo kuna baadhi ya wachezaji wachache wa ndani wamekuwa wakisajiliwa kwenda Klabu za Simba, Yanga, Azam na zingine, na usajili umekuwa na tija licha ya kwamba mwanzoni ulionekana wa kawaida tu na haukuwavutia mashabiki.

Mfano wa wachezaji ambao walichukuliwa poa ni Dickson Job kutoka Mtibwa Sugar, Bakari Mwamnyeto kutoka Coastal Union, Mudathir Yahaya mchezaji huru na Ibrahim Abdallah Hamad 'Bacca' kutoka KMKM ya Zanzibar, wote wakisajili na Yanga kwa misimu tofauti.

Kwa upande wa Simba ni Kibu Denis kutoka Mbeya City, Israel Mwenda, Hussein Abel wote kutoka KMC, Hussein Kazi kutoka Geita Gold.

Azam nao waliwasajili Nathaniel Chilambo kutoka Ruvu Shooting, Idd Nado kutoka Mbeya City ambayo nayo ilimsajili kutoka michuano ya Ndondo Cup, Sospeter Bajana na wengineo.

Ni sajili zilizoonekana za kawaida kwa sababu ni wazawa, lakini kwa sasa wameonekana kufanya vema, wengine kuwa nyota kwenye klabu zao.

Kipindi hiki cha dirisha dogo, pamoja na kuwapo kwa usajili wa wachezaji wa kigeni, lakini wapo Watanzania wachache ambao wanatajwa kwenye usajili kutoka klabu moja kuhamia nyingine.

Katika makala haya tumekusanya tetesi za usajili wa wachezaji wazawa ambazo hazijathibitishwa na klabu, lakini vyanzo zinaeleza zipo katika hatua za mwisho kukamilika...

**1. Edwin Barua - (Simba)**

Klabu ya Simba inatajwa kuwa kumsajili mchezaji huyu kutoka Prisons na inachosubiria ni kumtangaza tu.

Winga huyo wa zamani wa DTB ikiwa Ligi Daraja la Pili na baadaye kubatizwa kuwa Singida Big Stars kabla ya ubatizo wa tatu na kuwa Singida Fountain Gate, amekuwa kwenye kiwango cha juu kwenye Ligi Kuu msimu huu kiasi cha kupata dili kwenye klabu moja nchini Norway, lakini Simba ikaingia kati na kumpa mkataba wa miaka miwili, ni suala la muda tu.

**2. Ralients Lusajo - (Azam FC)**

Alianza mwenyewe kwanza kutangaza kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa anaondoka Klabu ya Namungo kwenda kusaka malisho sehemu nyingine. Lusajo ambaye ni mmoja wa mastraika wanaojua kufunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwahi kuhudumu pia katika timu ya KMC, anatajwa kuwa huenda akaibukia Azam FC, licha ya tetesi za awali kuwa atakwenda Singida Fountain Gate.

**3. Shiza Kichuya - (JKT Tanzania)**

Inatajwa kuwa anamaliza mkataba wake Klabu ya Namungo msimu huu huku akivutana na waajiri wake kuhusu dai la usajili.

Habari kutoka Klabu ya Maafande wa JKT Tanzania zinaeleza iko katika hatua nzuri ya kumnasa winga huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Simba, kabla ya kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, akarejea tena Simba, safari hii hakuwaridisha mabosi wa klabu hiyo akapelekwa Namungo kwa mkopo na ulipoisha akapatiwa mkataba wa miaka miaka miwili unaomalizika msimu huu.

**4. Ladack Chasambi - (Simba)**

Ameshaagwa rasmi na Klabu ya Mtibwa Sugar ambayo imemtakia kila la kheri katika klabu yake mpya. Mtibwa Sugar haikutangaza klabu ambayo imevunja mkataba baina yao na Chasambi, lakini habari zinaeleza kuwa Simba iko nyuma ya mpango huo.

Chasambi mwenye uwezo wa kucheza winga zote mbili, na kiungo mshambuliaji aliyepandishwa msimu huu kutoka kikosi cha pili cha Mtibwa Sugar, amekuwa na kiwango bora karibuni kila mechi za ligi anazocheza msimu huu.

**5. Ally Ally - (Mashujaa FC)**

Huyu ni beki wa kati wa zamani wa klabu mbalimbali nchini ikiwamo Yanga, Stand United na zingine nyingi. Anatajwa kutua Mashujaa FC, katika kipindi hiki cha dirisha dogo kwenda kuimarisha safu ya ulinzi.

**6. Chrispin Ngushi - (Singida Fountain Gate)**

Moja kati ya sajili zinazoweza kufanyika kipindi hiki cha dirisha dogo ni kwa straika huyo wa Yanga, Ngushi kuelekea Klabu ya Singida Fountain Gate.

Inaelezwa kuwa ni mmoja wa wachezaji wanaoweza kuondoka kwenye klabu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo, ama kwa kuachwa au kwa mkopo kutokana na kutokuwa na namba ya kudumu kikosini hapo.

**7. Gamba Matiko - (JKT Tanzania)**

Inawezekana kabisa kuwa Klabu ya JKU inajuta kushiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu.

Huenda kama isingeshiriki, mfano nafasi yake ingechukuliwa na Zimamoto, Gombani, au Taifa Jang'ombe wachezaji wake wasingeonekana na kuwa kivutio kwa klabu mbalimbali ambazo zimeanza kuwasomba.

Achilia mbali Yanga kumsajili Shekhan Ibrahim kabla hata ya michuano hiyo, Simba imemchukua Saleh Karabaka, lakini nahodha wake, straika Gamba Matiko inasemekana yupo katika hatua za mwisho kujiunga na JKT Tanzania.

**8. Yacoub Suleiman - (JKT Tanzania)**

Golikipa wa JKU Yacoub Suleiman naye inasemekana kama mambo yatakwenda kama yalivyopangwa ataibukia Klabu ya JKT Tanzania. Ikumbukwe kuwa timu hizi zina uhusiano, zote ni za Jeshi la Kujenga Taifa kwa upande wa Bara na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa upande wa Visiwani, hivyo ni sawa tu la kuhamisha pesa mfuko mmoja kupeleka mwingine.

**JE, WAJUA?**



KATIKA kikosi cha wachezaji 27 wa Taifa Stars kilichotangazwa na Kocha Adel Amrouche kwa ajili ya Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, Beki wa Azam FC, Cyprian Thobias Kachwele ambaye alizaliwa 15/02/2005, ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi huku Himid Mao Mkami anayeichezea Tala'ea El Gaish ya Misri aliyezaliwa 05/11/1992 na Mbwana Ally Samatta (PAOK FC - Ugiriki) aliyezaliwa 23/12/1992 wao ndio wenye umri mkubwa zaidi kikosini hapo.



## HABARI DODOMA

# Serikali yagawa mbegu za alizeti za Bil. 8.5/-

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SERIKALI imeupatia Mkoa wa Singida mbegu za ruzuku za alizeti zenye thamani ya Sh. bilioni 8.5 ambazo zitasambazwa kwa wakulima mkoani hapo ili kuongeza uzalishaji bora na wenye tija.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa programu ya usambazaji wa mbegu za alizeti aina ya "record" uliofanyika mjini Singida.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, chama, taasisi, wakuu wa idara na wakulima kutoka katika halmashauri saba za mkoa wa huo.

Silinde alisema katika mgawo huo, Mkoa wa Singida umepewa tani 600 za mbegu bora za alizeti na tani 315 za mbegu chotara ambazo ni sawa na asilimia 42.8 ya mbegu zote zitakazosambazwa nchini zenye thamani ya bilioni 6.5.

Alisema kwa upande wa mbegu za uchavushaji tani 285 ambazo thamani yake ni Sh. bilioni 2.28 ambazo zitasambazwa kwa msimu huu wa kilimo, mkoa wa Singida utapewa mbegu za Sh. bilioni.8.5 ambazo zitatolewa kwa bei ya ruzuku ya serikali.

Silinde alisema kuwa Wizara ya Kilimo kwa msimu wa kilimo wa 2023/24 kupitia Wakala wa Mbegu (ASA) wanatarajia kusambaza jumla ya tani 2045 za mbegu bora za alizeti zilizothibitishwa.

Alisema pia itasambaza tani 700 za mbegu chotara ambazo zinaingizwa kutoka nje ya nchi na tani 625.4 zinapatikana kupitia kwa kampuni binafsi ndani ya nchi.

"Matarajio yetu kama wizara na serikali ni kuona mbegu hizo zinatumika ipasavyo kama ilivyokusudiwa ili kutimiza azma ya serikali ya uzalishaji wa mafuta ya kutosheleza nchini." amesisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliwaagiza wakuu wa wilaya kuhakikisha mbegu za ruzuku za alizeti, zinawafikia wakulima katika vijiji vyote ndani ya mkoa huo.

"Natoa wiki tatu kwa wakuu wa wilaya wote kuhakikisha mbegu hii inafika kwenye kila kijiji... maagizo haya yatolewe pia kwa maofisa kilimo wote," alisema. Serukamba pia aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha zoezi la usambazaji wa mbegu hizo linafanyika mara moja.

Serukamba aliwaelekeza wakulima hao kuongeza maeneo yao ya kilimo pia kila kaya kuhakikisha inalima zao la alizeti katika msimu huu wa kilimo na kutoa msisitizo kwa vijana kutumia fursa hiyo.

Alisema ili kuongeza uzalishaji wenye tija, wakulima wanapaswa kulima kwa kutumia mbolea bora ili kupata mazao mengi zaidi na hivyo kuwawezesha kupata faida zaidi.



Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoite Araman (kulia), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Seleman Mwend (wa pili kushoto), wakimkabidhi mtungi wa gesi wa Oryx mamalishe Sada Said (katikati), katika hafla ya ugawaji wa mitungi 700 kwa wananchi wa wilaya hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wanufaika mitungi ya gesi

**Na Mwandishi Wetu,**
IRAMBA

WAJASIRIAMALI wadogo wakiwamo mamalishe na babalishe wilayani Iramba mkoani Singida wamepewa msaada wa mitungi ya gesi 700 na majiko, ili waachane na matumizi ya mkaa.

Msaada huo umetolewa na kampuni ya Oryx Gas Tanzania ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuhifadhi mazingira kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kupikia.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Seleman Mwenda akimwakilisha Mbunge wa Iramba Magharibi ambaye ni Waziri wa Fedha, Dk.Mwigulu Nchemba.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ugawaji wa mitungi hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman, alisema msaada huo pia umelenga kuliunga mkono kundi hilo katika juhudi zao za kujiendeleza kiuchumi na kusogeza huduma karibu na jamii.

"Oryx Gas tunaamini ukipika kwa kutumia gesi inaleta maendeleo mengi kwa jamii yetu. Pia kupika kwa gesi ya Oryx ni kulinda mazingira kwa kuacha kukata miti. Zaidi ya yote ni kulinda afya ya wanawake kwa kuwaepusha kuvuta moshi na mvuke unaoathiri mapafu na afya yao unaotokana na kuni na mkaa," alisema.

Alisema kwa miaka mingi Oryx Gas imekuwa kampuni kinara katika kukuza matumizi ya gesi nchini na kuanzia mwaka Julai mwaka 2021 wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2032 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Alisema Oryx Gas inatekeleza juhudi za Serikali za kueneza matumizi ya nishati safi kwa wananchi kwani hiyo ndio ndoto kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan kuona matumizi ya nishati safi ya kupikia yanapewa kipaumbele.

Aidha, alimshukuru Dk. Nchemba kwa kuwa balozi mzuri wa kuleta maendeleo kwa wanawake na jamii kwa ujumla kwa kuiunga mkono Oryx Gas Tanzania katika mpango wa matumizi ya nishati safi mkoani Singida.

"Tunafurahi kumkabidhi mitungi ya gesi 700 kwa wakazi wa Iramba ambayo inathamani ya zaidi ya Sh. milioni 50. Nawashukuru sana kwa nafasi hii mliyonipa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Seleman Mwenda, alisema wamegawa mitungi hiyo kwa wajasiriamali hao ikiwa ni sehemu kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kuhimiza wananchi kutumia nishati safi ya kupikia.

Alisema kupika kwa gesi kunasaidia kutunza mazingira pamoja na afya hasa kwa wanaojihusisha na shughuli za upishi, huku akifafanua wamegundua misitu inateketea kwa sababu ya matumizi ya kupikia.

Alisema athari nyingi ambazo wanazipata baba na mama lishe zinatokana na mkaa pamoja na kuni na hivyo kuathiri afya zao.

# Waiangukia serikali kuboresha elimu kwa watoa huduma afya

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeombwa kuongeza kiwango cha utoaji elimu kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, hususani elimu ya uzazi wa mpango ili kuboresha huduma kwa wananchi katika maeneo ya vijijini.

Aziza Juma mkazi wa kijiji cha Mahomanyika jijini hapa, alisema hayo wakati wa mahojiano na gazeti la Nipashe kuhusu suala la uzazi wa mpango linalotolewa katika hospitali mbalimbali nchini.

Alisema uzazi wa mpango ni jambo la muhimu sana wananchi kulijua kwa sababu linapunguza changamoto ya wanawake kuzaa bila mpangilio na kushindwa kuwapa malezi bora watoto wao.

Kutokana na hilo aliomba serikali kuweka mkazo wa utoaji elimu kwa wahudumu ngazi ya jamii ili watoe elimu kwa kinamama kuhusu matumizi sahihi ya uzazi wa mpango.

Alisema, wahudumu hao ni watu muhimu sana kwa jamii kwa sababu hukutana na wanawake wajawazito na kuwaeleza changamoto zao nao huziwasilisha katika vituo vya afya ili ziweze kufanyiwa kazi.

Mwananchi mwingine, Salama Ally, alisema wahudumu ngazi ya jamii ndio kila kitu hivyo serikali inapaswa kuzingatia kuwapa elimu zaidi ya ujuzi ili nao wakaitoe kwa wananchi hususani wa vijijini.

Hata hivyo, alilipongeza Shirika la Maria Stoppers kutokana na jitihada za kuzunguka mikoani kwa ajili ya kuzungumza na jamii juu ya masuala mbalimbali yakiwamo ya uzazi wa mpango.

Naye Dk. Julieth Kabengula alisema malezi ya watoto yanapaswa kuzingatia katika suala la uzazi wa mpango.

Alisema ili kuwaepusha watoto na magonjwa mbalimbali ikiwamo ukeketaji mzazi anapaswa kuzingatia malezi bora ya watoto ambayo yanakwenda sambamba na uzazi wa mpango.

"Nawashauri kinamama wazingatie suala zima la uzazi wa mpango ili wawe na familia bora. Kadhalika, alisema jamii haipaswi kuogopa kutumia njia za uzazi wa mpango ili kuwa na familia bora ambazo wanaweza kuzihudumia.

Alisema kuna njia nyingi za uzazi wa mpango hivyo kila mmoja anapaswa kuchagua atumie ipi ambayo anaona ni sahihi kwake.

Hata hivyo, alisema wasisikilize maneno ya mtaani kuwa njia za uzazi wa mpango zina madhara hiyo sio kweli kwani ni salama kwa jamii.



## Makubaliano mradi Liganga, Mchuchuma mbioni kukamilika

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI imesema iko mbioni kukamilisha mazungumzo na mwekezaji wa mradi wa Liganga na Mchuchuma uliopo wilayani Ludewa katika Mkoa wa Njombe kwa kuzingatia sheria ya mapitio na majadiliano kuhusu mkataba yenye masharti hasi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, aliyasema hayo juzi wakati alipotembelea eneo la mradi huo.

Alisema mazungumzo hayo yanakwenda sambamba na kuhakikisha rasilimali za nchi zinatumika kuongeza pato la taifa na kuleta maendeleo.

"Sasa ni dhamira ya dhati kabisa ya kusema kwamba mradi unakwenda kuanza tunayo malengo kwenye Ilani yetu ya chama ya mapinduzi lakini pia katika maono yetu ya 2025 tumeeleza wazi huu ni mradi muhimu," alisema Dk. Chana.

Dk. Chana alisema watahakikisha mazungumzo hayo yanakwenda vizuri kwa kuwa Watanzania wanayo kiu ya kuona mradi huo wa kimkakati wa Liganga na Mchuchuma unaanza mara moja.

"Sisi Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na waziri mwenzangu anayesimamia masuala la viwanda tunaendelea kusimamia suala hili kwa karibu sana," alisema Waziri Dk. Chana.

Pia Dk. Chana alibainisha kwamba lengo la serikali ni kuhakikisha mradi huo unawanufaisha Watanzania wote kama sheria zinavyoelekeza maliasili za taifa zinapaswa kutumika kwa manufaa na faida ya Watanzania wote.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Uangalizi na Utajiri wa Rasilimali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Neema Mwanga, alisema mchakato wa mradi huo upo kwenye mazungumzo ili kupitia sheria za mikataba.

"Mnamo mwaka 2017 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mbili, sheria ya mamlaka ya nchi kuhusu umiliki wa utajiri na maliasili za nchi na sheria ya mapitio na majadiliano kuhusu mikataba yenye masharti hasi," alisema Mwanga.

Alisema Sheria ya Mapitio na Majadiliano inataka mikataba yote inayoingiwa na wawekezaji katika uchimbaji au uvunaji na matumizi ya utajiri na mali asili za nchi ilenge katika kuhakikisha rasilimali zinapatikana zinaongeza pato la taifa na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

Aidha, alisema kuwa kwa sababu nchi inahitaji wawekezaji, hivyo ni lazima mikataba inayoingiwa iwe na tija kwa sababu sheria zimesisitiza.

Meneja Mradi wa Liganga na Mchuchuma kutoka Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Dk. Witness Ishuza, alisema kwa mujibu wa tafiti zilizofanyika katika eneo la Liganga kuna tani zaidi ya milioni 128 za chuma.

# Baraza la Machifu laingilia kati mgogoro urithi wa mali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BARAZA la Machifu wa Kabila la Wasangu wilayani Mbarali mkoani Mbeya, limeingilia kati mgogoro wa kugombea mali za urithi baina ya watoto wa marehemu Edward Mwangonela wanaoishi katika Kata ya Ruiwa.

Mwangonela alikuwa miongoni mwa watu maarufu katika Kata ya Ruiwa na alifariki hivi karibuni na kuacha mali mbalimbali ikiwamo mifugo na mashamba hali iliyosababisha watoto wake kuanza kugombea mali hizo na kutishiana kuuana.

Wakizungumza kwenye kikao cha baraza hilo ambacho kiliwahusisha pia vijana wanaogombea mali hizo, wazee hao wa mila waliwataka kuacha kutishia kumwaga damu na badala yake wafuate taratibu za kisheria kutatua mgogoro huo.

Chifu Mkuu wa Kabila la Wasangu, Chifu Mhomela Melele, aliwaelekeza vijana hao kufuata taratibu za kisheria kutatua mgogoro huo na asingependa kusikia tukio lolote la umwagaji damu kwenye himaya yake. Alisema baba wa vijana hao alihamia katika eneo hilo na kukaribishwa kwa upendo na aliishi kwa amani na wenyeji hali iliyomfanya kuwa miongoni mwa watu maarufu kwenye eneo hilo.

Alisema mali alizotafuta baba zisiwe chanzo cha kuvunjika amani kati yao wakati wao wapo na na kuwasihi vijana hao kuacha mara moja kutishiana.

"Nikija kusikia kuna mmoja wenu ameuawa kwenye hii familia, nawahakikishia kwamba tutachukua hatua ambazo hamtakuja kuamini, baba yenu tuliishi naye kwa amani sana na tulimpokea wenyewe tukampa haya maeneo ambayo mnagombea," alisema Chifu Melele.

Mzee Shadrack Sange ambaye ni mjumbe wa baraza hilo aliwaelekeza vijana hao kila mmoja kujitafutia mali zake binafsi na kuacha kugombea mali za baba yao kwa kutishiana kumwaga damu.

Alisema wakati wa uhai wake baba yao vijana hao hakuwahi kufanya tukio lolote ambalo lilikuwa baya na hivyo wanashangaa tabia ambazo vijana hao wanazionyesha mbele ya jamii.

Alisisitiza kuwa endapo vijana hao wataendelea kuonyeshana ubabe, baraza hilo litafanya uamuzi ambao utawafanya wajutie katika maisha yao na akawataka kutoa taarifa kama vitisho hivyo vitaendelea.

Wakizungumza mbele ya baraza hilo, vijana hao walisema chanzo cha kutoelewana ni baadhi ya wanafamilia kutaka kuhodhi mali zote za marehemu baba yao.

Mmoja wa vijana hao, Shaban Mwangonela alisema baba yao alikuwa na wake wengi na kwamba mpaka anafariki aliacha watoto 22 ambao baadhi yao ni wakubwa na wanajitegemea na hivyo wanataka kuzimiliki mali zote.

Aliwaomba viongozi wa mila na wa serikali katika eneo hilo kuendelea kuwasaidia kutatua mgogoro hilo ili uishe na waendelee kuishi kwa amani.

Naye Alphonce Mwangonela ambaye ni miongoni mwa wanaodaiwa kuwatishia wenzake aliwaomba wenzake kutatua mgogoro huo kwa kwa njia ya amani badala ya kuendelea kuviziana akidai kuwa watasababisha mambo mabaya.

Alisema ili kutatua mgogoro huo ni vema wakatumia njia za kisheria ikiwemo kwenda mahakamani badala ya kuendelea kutishiana bila kupata suluhu ya kudumu.



Baadhi ya wajasiriamali wa ndizi katika Soko la Matema, wilayani Kyela, mkoani Mbeya wakisubiri wateja mwishoni mwa wiki.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbeya yamaliza kero wanafunzi kukaa chini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la wanafunzi wa shule za msingi kukaa chini katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, limemalizika baada ya halmashauri hiyo kutengeneza zaidi ya madawati 6,200 ambayo yalikuwa yanahitajika na kuyasambaza kwenye shule zilizokuwa na uhaba.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Nchimbi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wakati shule zinapofunguliwa leo nchini kote.

Nchimbi alisema madawati hayo yamewayatengeneza kwa gharama ya Sh. milioni 186 ambazo zimetokana na mapato ya ndani ya jiji hilo na wanaendelea na utekelezaji wa miradi mingine.

Aidha, alisema katika kipindi cha likizo wametumia zaidi ya Sh. milioni 80 kukarabati vyumba vya madarasa vilivyokuwa vimechakaa katika shule nne za msingi ambavyo vilikuwa na hali mbaya.

Alizitaja shule zilizonufaika na ukarabati huo kuwa ni Shule ya Msingi Isanga, Simike, Nsoho na Mwasanga ambazo sasa wanafunzi watasomea katika mazingira mazuri.

"Lakini pia tumetumia zaidi ya Sh. 406 kujenga vyoo katika shule za msingi ambazo zilikuwa hazina miundombinu hiyo na sasa wakati shule zinafunguliwa watoto wetu watakuwa na vyoo bora," alisema Nchimbi.

Alizitaja shule ambazo zimenufaika na ujenzi wa vyoo kuwa ni Inyala, Mwasanga, Simike, Nsongwi, Mabonde, Halinji, Ikulu, Uhuru, Gombe, Tambuka Reli, Mapambano, Lyoto, Ikuti, Muungano na Igale.

Alisema baadhi ya shule hizo zilikuwa zinakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo na zingine zilikuwa hazina na hivyo wanafunzi walikuwa wanasomea kwenye mazingira ambayo yalikuwa siyo rafiki kiafya.

Vilevile alisema katika baadhi ya shule wamekamilisha ujenzi wa nyumba za walimu ikiwemo shule ya Msingi Nsoho ambayo walitumia Sh. milioni 10 kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mwalimu.

Baadhi ya wadau wa elimu jijini humo walisema shule zao zinakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanahitaji ushirikiano kati ya wazazi na serikali kuyatatua ili sekta ya elimu iendelee kuwa bora.

Mmoja wa wadau hao, Lydia Kamwelwe, alisema shule nyingi katika jiji hilo zimechakaa na hivyo zinahitaji ukarabati mkubwa ili ziendane na hadhi ya jiji hilo.

Alisema hivi sasa serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari ambavyo viko katika hali nzuri na hivyo kuifanya miundombinu ya zamani kuonekana chakavu kupita kiasi.

Aliiomba serikali pamoja na wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kukarabati vyumba vya madarasa na miundombinu mingine kwenye shule ili wanafunzi wasome katika mazingira yanayofanana.



# Wanawake wahimizwa kugombea nafasi za uongozi serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI mstaafu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Sophia Simba, amewahimiza wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi ili kufikia asilimia 50 kwa 50 katika ngazi za uamuzi na kutunga sheria.

Akifungua Kongamano la Wanawake UWT visiwani Zanzibar jana, Sophia aliwataka wanawake kuondoa woga na kugombea nafasi mbalimbali katika majimbo ili kufikia malengo waliojipangia.

Alisema kuwa, jukumu la kufikisha asilimia 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi ni la wanawake wenyewe hivyo watumie utaalamu wao kuhakikisha wanapata fursa za kugombea na wanawake ni jeshi kubwa.

Aidha alisema kongamano hilo, litasaidia jamii kupata fursa ya kutafakari, wanawake walipotoka, walipo sasa na wanapokwenda ili kupiga hatua, zitakazoweza kufikia malengo ya Mapinduzi sambamba na kujifunza historia ya nchi na Chama Cha Mapinduzi.

Simba alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa kuyalinda na kuyaendeleza Mapinduzi ya miaka 1964 pamoja na kudumisha amani na utulivu iliopo nchini.

Hata hivyo alisema kwa kutambua mchango wa viongozi waasisi wanawake wa CCM katika kushiriki na kuunga mkono jitihada za kudumisha Mapinduzi jambo ambalo limetokana na uzalendo walioonyesha wakati wa kupigania ushindi.

"Tunatambua mchango wa wanawake walioshiriki katika kuunga mkono jitihada za Mapinduzi na kufanya kazi kwa Uzalendo na kuweza kupigania ushindi wa nchi yetu," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Taifa (UWT) Jokate Mwegelo, alisema lengo la kuundwa UWT ni kuwatambua wanawake, kuandaa mikakati yao na kutafuta fursa mbalimbali zilizopo ili kuleta usawa na kuondokana na mfumo dume.

Baadhi ya washiriki wa kongamano hilo, walisema wamepata kujua historia ya Mapinduzi na umuhimu wa kuyalinda na kuwa wazalendo wa kujenga nchi yao na kuomba kuandaliwa kongamano kama hilo mara tatu kwa mwaka na sio kusubiri Maadhimisho ya Mapinduzi pekee.



Baadhi ya washiriki wa kongamano la wanawake UWT wakishangilia katika kongamano lililofunguliwa na Mwenyekiti Mstaafu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Sophia Simba, jana visiwani Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za Miaka 60 ya Mapinduzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoteli kubwa ya kitalii yazinduliwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, jana aliweka jiwe la msingi katika mradi wa hoteli kubwa ya kitalii ijulikanayo kama Tulia Pamunda Resort Island iliyopo katika Kisiwa cha Pamunda, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za miaka 60 ya Mapinduzi.

Hoteli hiyo inayomilikiwa na wageni kutoka nchi za Czech Republic inaelezwa ikikamilika itakuwa inapokea matajiri wakubwa ulimwenguni kwa gharama ya Sh. milioni 13 kulala kwa siku moja.

Akizungumza katika hafla hiyo, waziri huyo alisema kisiwa hicho ni miongoni mwa 16 vilivyopo Unguja na Pemba vilivyokodishwa na serikali kwa wawekezaji baada ya kuona vimekaa kwa muda mrefu bila ya kuendelezwa na kushindwa kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa kulinda rasilimali zilizopo pamoja na maslahi ya wananchi katika miradi inayotekelezwa katika visiwa vidogo pamoja na maeneo mengine.

Jamal alisema serikali imetunga sheria mpya ya uwekezaji ya mwaka 2023 na sasa ipo katika hatua za mwisho za utiwaji saini ili kuanza utekelezaji wake, ambayo imeweka masharti kwa wawekezaji ili kulinda rasilimali zikiwamo visiwa vidogo.

"Sheria pia imetoa fursa kwa ushiriki wa wananchi katika shughuli za uwekezaji ikiwamo kupatiwa fursa za ajira kwa wananchi wanaozunguka miradi hiyo, wawekezaji kuchangia uendeshaji wa huduma za kijamii katika maeneo ambayo miradi hiyo inayofanyika, " alisema Waziri huyo.

Hata hivyo alisema uamuzi wa wawekezaji hao kuendelea kuwekeza Zanzibar, ni kutokana na uzuri wa visiwa hivyo pamoja na imani kubwa waliyonayo kwa serikali na sera zake nzuri zenye lengo kutoa matumaini kwa kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliitaka wizara inayosimamia uwekezaji kusimamia vizuri utekelezaji wa sheria hiyo mpya ili kuleta matunda yaliyokusudiwa kwa wananchi.

Aliipongeza Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa kusimamia vizuri mchakato mzima wa ukodishwaji wa visiwa na kuiagiza kuendeleza kasi hiyo katika utekelezaji wa miradi ya visiwa pamoja na miradi mengine kwa maslahi ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema Zanzibar ina visiwa 52 na hadi sasa imeshakodisha visiwa 16 ambapo hayo ni mafanikio makubwa.

Alisema pia kwa mara ya kwanza hoteli yenye hadhi ya nyota saba inayoitwa Mantuli inatarajiwa kujengwa Kisiwani Pemba, ambapo kwa Afrika itakuwa ni hoteli ya kwanza yenye hadhi hiyo.

Sharif alisema katika Hoteli ya Tulia Pamunda Island kutakuwa na mchezo mkubwa wa kitajiri duniani unaoitwa Formula one hivyo marajiri wakubwa watafika katika kisiwa hicho.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya nane ya uongozi wa Dk. Mwinyi imekuwa na miradi ya uwekezaji 269 ambayo inamtaji wa dola bilioni 4.5 na italeta ajira 17,000 ambapo ni maendeleo makubwa.

Mwekezaji wa mradi huo, Lucas Senegor, alisema Zanzibar ni kisiwa kizuri cha uwekezaji kinachosifika duniani hasa katika sekta ya utalii na visiwa vyenye mandhari mazuri ya kuwavutia wageni.

Alisema mpaka hoteli hiyo itakayokuwa na uwezo wa kushindana na hoteli kubwa duniani utakapokamilika itagharimu jumla ya Sh. bilioni 76 na itaajiri watu 300.

Kisiwa cha Pamunda kipo Jimbo la Dimani Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ambapo ujenzi wa hoteli unandelea kisiwani humo na ni mwendo wa dakika 20 kutoka katika Bahari ya Bweleo hadi kufika kisiwani humo kwa usafiri wa baharini.

# Wanataaluma watakiwa kutumia mapinduzi kuchochea maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema wanataaluma nchini wanapaswa kuendeleza dhana ya mapinduzi ili kuchochea maendeleo ya nchi na kuongeza uelewa kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Alisema hayo jana akifungua kongamano la kitaaluma lililofanyika katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Tunguu Wilaya ya Kati Unguja lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Alisema historia ya mapinduzi inadhana pana hivyo ni vyema wanataaluma kuisoma na kuichambua kwa kina ili kuimarisha misingi ya kufanyika kwa mapinduzi hayo na kuepusha upotoshaji.

Alisema lengo la mapinduzi ni kuwaweka watu wote sawa hivyo ni vyema kuendelezwa dhana hiyo kwa ajili ya maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye.

Aidha aliwataka wanafunzi hao kulitumia kongamano hilo vizuri kwa kuzungumzia dhamira na malengo ya mapinduzi hayo badala ya kuwapa fursa watu wenye nia ovu ya kupotosha mapinduzi hayo.

Alisema kabla ya kufanyika kwa mapinduzi hakukuwa na fursa kwa wananchi kupata elimu hivyo baada ya mapinduzi hayo kumekuwa na mwamko kwa Wazanzibari kupata fursa ya kuanzishwa kwa vyuo hivo ili kuimarisha ustawi wa sekta ya elimu na kuweka misingi imara ya uchumi.

Waziri huyo alisema dhana ya mapinduzi inakwenda kwa vitendo ikiwamo kuongezeka kwa uchumi, vyuo vikuu sambasamba na kuchochea maendeleo ya mtu mmoja na kuleta ustawi kwa watu wote. Aidha alisema serikali zote mbili zimeweka mkazo wa kupatikana kwa elimu kwa watu wote bila ya ubaguzi wa rangi wala dini hatua ambayo inakwenda sambamba na malengo ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema kazi kubwa ya vyuo vikuu ni kuchechemua fikra za mapinduzi pamoja na elimu kwa ujumla.

Makamu Mkuu wa SUZA, Profesa Mohamed Makame Haji, alisema kabla ya Mapinduzi hakukuwa na vyuo vikuu ambapo Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) kilijengwa 2001 ambapo ni sehemu moja ya kujivunia uwepo wa mapinduzi hayo. Alisema tangu kuanzishwa kwa chuo kikuu, Zanzibar imepata mafanikio ikiwamo masuala ya utafiti na kuwapata wasomi wabobezi wenye uwezo na uweledi mkubwa wa kuleta mageuzi ya kimaendeleo.

Akitoa mada ya wasifu na sifa za Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume, Naibu Katibu Mkuu Mstaafu, Abdalla Juma Sadala, alisema alikuwa kiongozi anayependa kushirikisha watu katika mambo muhimu ili kuleta umoja hasa katika ukombozi.

Akiwasilisha mada ya uchumi mkuu wa sayansi asilia na sayansi jamii, Abdalla Mkumbukwa kutoka SUZA, alisema Mzee Abeid Karume katika kuinua uchumi ameanzisha Benki ya Watu wa Zanzibar na watu kuitumia kuweka amana zao.

Alisema Karume alitoa fursa kwa watu kuwapa ardhi kwa ajili ya kulima mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara ili kukuza uchumi wao.

# Wimbi wizi wa pikipiki laibuka vijiji vya mpakani

Na Samson Chacha, TARIME

WAKAZI wa vijiji vya mpakani mwa Tanzania na Kenya wameziomba serikali za Tanzania na Kenya kushirikiana kudhibiti wimbi lilioibuka la wizi wa pikipiki na kuvushwa nchi nyingine.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti katika miji ya Tarime, Sirari, Kubiterere, Ikoma, Kogaja, Borega na Shirati wananchi hao walisema wimbi la wizi huo ni kubwa.

Wengine walioibiwa mwishoni mwa mwaka jana ni Mangera Chacha na Charles Joseph, ambao wameripoti matukio hayo polisi, lakini mpaka sasa hawajapata pikipiki zao.

Mwandishi wa habari Jumanne Ntono, alisema aliibiwa pikipiki yake na kijana mmoja kutoka vijiji vya mpakani aliyefika ofisini kwake na kumtuma dukani na kutokomea na usafiri wake na fedha alizompa kununulia bidhaa.

Wananchi hao wameliomba Jeshi la Polisi mpakani pande zote mbili Tanzania na Kenya kushirikiana kufanya msako wa pikipiki zisizo na kadi ili kubaini uhalali wake.

"Pikipiki nyingi zimeripotiwa kuibwa na wimbi hilo limeshamiri mpakani hatua zaidi zichukuliwe ili kukomesha na kuwakamata wahusika na kufikishwa mahakamani," alisema mmoja wa wananchi hao.

Madiwani wa vijiji vya mipakani, Amos Sagara, Kata ya Sirari, Petro Ntogoro, Kata ya Mwema, Nashon Mchuma Kata ya Gwitiryo na John Bosko Mbusiro, Kata ya Regicheri, wameziomba serikali za nchi hizo mbili kushirikiana kufanya msako wa kuwakamata wezi hao.

Isebania Kenya, Mwenyekiti wa Haki za Binadamu Wilaya ya Kurya, West Masaithe alisema zaidi ya pikipiki 20 waliokopeshwa na zimeibwa kwa miezi mitatu na kuvushwa kuja Tanzania. "Tunaomba Polisi Tanzania kufanya msako na kubaini pikipiki zilizo halali na kukamata ambazo hazina kadi za kununulia kwani nyingi zimeibiwa," alisema mwenyekiti huyo.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert, akichimba shimo kwa ajili ya kupanda mti eneo la kituo cha wazee cha Ipuli Tabora juzi. Shirika hilo kwa kushirikiana na wanafunzi wa vyuo mbali mbali lilipanda miti 145 ya matunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Washindi kampeni ya NMB wajazwa noti

Na Mwandishi Wetu

KAMPENI ya 'Weka, Tumia na Ushinde' inayoendeshwa na Benki ya NMB, ikilenga kuhamasisha matumizi yasiyo ya fedha taslimu, imezidi kuchanja mbuga, baada ya juzi kuchezeshwa kwa droo ya tisa iliyotoa washindi 100 waliojinyakulia Sh. milioni 10 (Sh. 100,000 kila mmoja).

Idadi ya washindi 100 wa droo hiyo inafanya wateja wa benki hiyo waliojinyakulia zawadi za wiki kufikia 900 kati ya 1,200 wataotarajiwa kujishindia Sh. 100,000 kila mmoja katika kipindi cha miezi mitatu ya kampeni hiyo ijulikanayo kama 'NMB MastaBata Halipoi'. Ilizinduliwa Oktoba 27 mwaka jana.

Ukiondoa washindi 1,200 wa kila wiki, NMB MastaBata Halipoi - kampeni yenye zawadi mbalimbali zenye thamani ya Sh. milioni 350, inatoa pia washindi 30 wa mwisho wa mwezi (washindi 15 kwa kila mwezi wanaojizolea Sh. 500,000 kila mmoja), washindi 240 wa papo kwa papo wanaopata Sh. 50,000 kila mmoja.

Akizungumza wakati wa droo hiyo iliyoendeshwa chini ya usimamizi na Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Rasuli Masudi, Meneja wa NMB Tawi la Magomeni, ilikochezeshwa droo hiyo, Mary Marungi, alisema wateja wa papo kwa papo wanaopewa zawadi ni wale watakaokutwa wanafanya ununuzi kwa kadi.

"Pia tunawazawadia washindi 10 na wenza wao ambao wapata fursa ya kwenda kuhudhuria Tamasha la NMB Full Moon Party linalofanyika Kendwa Rocks Hotel, Zanzibar, safari iliyogharamiwa kila kitu na NMB, pamoja na kupewa fedha za matumizi binafsi ya Sh. 200,000 kila mmoja.

"Kampeni hii itahitimishwa kwa washindi 12 na wenza wao kufanya safari ya utalii mjini Cape Town, Afrika Kusini, gharama zote zikiwa zimelipiwa na NMB, ambako watakula bata kwa siku tano," alisema Marungi wakati wa ufunguzi wa droo hiyo iliyoambatana na zawadi kwa wateja waliokuwa wanapewa huduma katika tawi hilo.

Marungi alibainisha kuwa nia ya NMB MastaBata Halipoi ni kuifanya jamii kuendana na kasi ya teknolojia, wanakowapa msisitizo wa kufanya ununuzi na malipo kwa kutumia NMB MasterCard, Lipa Mkononi (QR Code) na Vituo vya Mauzo (PoS) na malipo ya mtandaoni na yale ya kwenye vituo vya mafuta, 'supermarket' na migahawa mbalimbali.

Masudi kutoka GBT aliipongeza NMB kwa kudumisha utamaduni chanya wa kuzawadia wateja wao waliouanza mwaka 2018 ilipozindua kampeni hiyo na kwamba wateja wa benki hiyo wanapaswa kushiriki matumizi ya kadi ili kujihakikishia nafasi za kushinda fedha taslimu na safari za kitalii ndani na nje ya nchi.

"Sisi GBT tunawapongeza NMB kwa hiki inachofanya kwa msimu wa tano sasa, inaonesha namna inavyowajali wateja wao kwa kuwazawadia kila wanapoweka akiba na wanapofanya matumizi. "Jukumu letu ni kusimamia na tunawahakikishia wote kwamba droo hizi zinafanyika kwa kufuata vigezo na masharti, hakuna ujanjaujanja," alisema Masudi.

Droo hiyo ya tisa iliyoshuhudiwa pia na Meneja wa Kitengo cha Kadi NMB, Sophia Mwamwitwa na Meneja Huduma za Kadi NMB, Ednamamu Mshubi, imefanyika wiki moja tu tangu wateja 15 walipojinyakulia zawadi ya Sh. 500,000 kila mmoja katika droo ya pili ya mwisho wa mwezi iliyofanyika Desemba 29 jijini Arusha.

# SMZ kuendeleza mazingira mazuri kufundishia

Na Sabato Kasika

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imeahidi kuendelea kuboresha upatikanaji wa elimu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati akiweka jiwe la msingi la Shule ya Msingi ya Kidichi ikiwa ni shamra shamra za sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar juzi.

Alisema, ujenzi wa shule hiyo ni mojawapo ya hatua ya kutekeleza azma ya ya serikali ili visiwa vya Zanzibar vipate huduma mbali mbali ikiwamo elimu bora na wataalamu wenye uwezo wa kuchangia maendeleo ya nchi.

Alisema serikali inatambua changamoto ya uhaba wa nafasi katika shule nyingi kuendeshwa kwa mfumo wa mikondo miwili kwa baadhi ya wanafunzi kusoma asubuhi na wengine mchana, hali inayokwamisha ufanisi katika ufundishaji na kudhoofisha maendeleo ya elimu kwa vijana.

"Changamoto hii inatokana na kasi kubwa ya idadi ya watu, kwani takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita idadi ya wakazi wa Zanzibar imeongezeka kutoka milioni 1.3 hadi kufikia milioni 1.8 ikiwa ni ongezeko la wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka," alisema Riziki.

Alisema, uamuzi wa serikali wa kuimarisha ubora wa elimu ni sehemu ya mkakati madhubuti katika kufikia malengo yaliyoainishwa katika dira ya maendeleo ya 2050 na kuongeza kuwa bila ya kuwa na elimu bora inayokwenda sambamba na mabadiliko ya ulimwengu itakuwa ni vigumu kufikia malengo ya dira ya 2050.

Alisema hayo yanafanyika ikiwa ni kumwezesha kijana wa kizanzibari kushindana vyema katika soko la ajira la kitaifa, kikanda na kimataifa na muhimu kwa kila mmoja kuwajibika si kuwaandikisha watoto pekee, pia kufuatilia kwa karibu maendeleo yao ya kielimu.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulghulam Hussein alisema ujenzi wa shule hiyo ni miongoni mwa mpya 25 zinazojengwa Unguja na Pemba, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za kutoa huduma bora za elimu na pia kuifanyia matengenezo Shule ya Msingi ya Kidichi ili iwe ya kisasa kwa lengo la kutoa elimu bora.

Akitoa taarifa ya kitaalamu, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Dk. Mwanahamis Adam Ameir, alisema shule hiyo ilianza kujengwa Mei mwaka jana na inatarajiwa kumalizika mwaka huu ikiwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya nane.

Shule hiyo ni ya ghorofa mbili ambayo ina madarasa 29, vyoo 25, ofisi nne za walimu, ukumbi mmoja wa kufanyia mitihani, maabara, chumba kimoja cha TEHAMA na maktaba moja, huku gharama yake ikiwa ni Sh. bilioni 4.5.

# Marekani yaisisitiza Burundi kuheshimu haki za binadamu

**GITEGA, Burundi**

MAREKANI imetoa wito kwa Burundi kuheshimu haki za binadamu huku ikieleza kutatizwa na kauli ya Rais wa taifa hilo, Evariste Ndayishimiye, ambaye wiki iliyopita aliwataka raia kuwapiga mawe watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Aidha, awali Marekani iliweka vikwazo mbalimbali vikiwamo vya usafiri na kuiondoa Uganda katika mkataba wa biashara usio na ushuru, kutokana na sheria yake iliyoipitisha dhidi ya wapenzi wa jinsia moja.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller, katika taarifa iliyotolewa jana alisema taifa hilo linatatizwa mno na matamshi hayo yanayowalenga Waburundi walio kwenye mazingira magumu na waliotengwa.

Miller alitoa wito kwa viongozi wa Burundi kuheshimu utu na upatikanaji sawa wa haki ya kila mwanajamii wa Burundi. Pia ilielezwa kuwa maoni ya Ndayishimiye yamezidisha ukandamizaji dhidi ya jamii hiyo katika taifa ambalo tayari


wanakabiliwa na ubaguzi wa kijamii na kifungo cha jela cha hadi miaka miwili iwapo watapatikana na hatia ya kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Rais Ndayishimiye akijibu swali kutoka kwa waandishi Desemba 29, 2023 alisema nchi zenye nguvu zinastahili kukaa na misaada yao iwapo misaada hiyo inaambatana na masharti ya kuwapa wapenzi wa jinsia moja haki.

Akiinukuu Biblia huku akisema Mungu anawachukia wapenzi wa jinsia moja na kufafanua kwamba hilo si tatizo tena Burundi.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa ni kinyume cha sheria kushiriki mapenzi ya jinsia moja Burundi na anayepatikana na hatia anaweza kuadhibiwa kwa kifungo cha hadi miaka miwili gerezani.

**DW**



Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud (katikati) akitia saini sheria kubatilisha mkataba wa maelewano kati ya Ethiopia na Somaliland, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Bangladesh yapiga kura uchaguzi uliosusiwa na upinzani

**DHAKA, Bangladesh**

WANANCHI wa Bangladesh wamepiga kura katika uchaguzi wa wabunge uliohakikishiwa kumpa Waziri Mkuu Sheikh Hasina muhula wa nne mfululizo, baada ya kususiwa na vyama vya upinzani.

Inaeleza kuwa hizo ni chaguzi ambazo matokeo yake yanaonekana tayari yameandikwa. Kutokana na kukosekana kwa chama kikuu cha upinzani na kwamba hali hiyo itatoa nafasi kwa waziri huyo aliyekuwa madarakani tangu 2009, kuongeza kwa mhula wa nne.

"Kushiriki uchaguzi chini ya Hasina, kinyume cha matarajio ya watu wa Bangladesh, kutadhoofisha matumaini ya wale waliopigana, kumwaga damu na kutoa maisha yao kwa ajili ya demokrasia," amesema kiongozi wa upinzani Tarique Rahman anayeishi uhamishoni.

Shahdeen Malik, ambaye ni msimamizi wa Kituo cha Majadiliano ya Sera, alisema chama kikuu cha upinzani kinazingatia kwamba serikali ambayo inadhibiti utawala mzima, itahusika na wizi wa kura.

Ilielezwa kuwa kutokana na kususia huko, chama cha Sheikh Hasina, hakina wapinzani kivitendo katika majimbo wanakogombea.

Lakini alishindwa kusimamisha wagombea katika wachache wao, kwa nia dhahiri ya kuzuia Bunge la umoja huo kuonekana kama chombo cha chama kimoja.

Baadhi ya wapigakura walisema walitishiwa kunyang'anywa kadi zao za manufaa za serikali, ili kupata manufaa ya kijamii, ikiwa watakataa kupigia kura chama tawala.

Hata hivyo ilielezwa kuwa chama kikuu cha upinzani cha Bangladesh Nationalist Party (BNP) na vyama vingine vilifanya maandamano mwaka jana kumtaka waziri mkuu kujiuzulu na kuendeleza serikali ya mpito isiyoegemea upande wowote

kusimamia uchaguzi huo, bila mafanikio.

Vile vile kwa mujibu wa upinzani nchini humo baadhi ya makada 25,000 wa upinzani, wakiwamo viongozi wote wa ndani wa BNP, walikamatwa katika wimbi la ukandamizaji. Na kwamba serikali kwa upande wake, iliripoti kukamatwa kwa watu 11,000.

**RFI**

# Makubaliano Ethiopia na Somaliland yabatilishwa

**SOMALILAND, Somalia**

RAIS wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, ametia saini sheria kubatilisha mkataba wa maelewano na mashirikiano ya bandari kati ya Ethiopia na Somaliland.

Mohamud alieleza kuwa sheria hiyo mpya ni dhihirisho la uwajibikaji wa Somalia katika kulinda umoja, uhuru na hadhi ya ardhi yake kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Sheria hiyo inaeleza kwamba, makubaliano yaliofikiwa kati ya serikali ya Ethiopia na Somaliland Januari 1, 2024 mjini Addis Ababa ni batili na hayana msingi wa kisheria, bali yanakwenda kinyume na katiba ya nchi, sheria za kimataifa kama ya Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU) na Katiba ya Jumuiya ya Maendeleo Afrika Mashariki na pembe ya Afrika (IGAD).

Kadhalika inaelezwa kuwa makubaliano hayo yanakiuka pia azimio la kimataifa la baraza la usalama linalodhibiti uhuru wa nchi, na sheria ya uwekezaji wa kigeni Somalia miongoni mwa sheria nyingine za nchi.

Hata hivyo, mzozo wa kidiplomasia kati ya Somalia na Ethiopia umeibuka baada ya Ethiopia kutia saini makubaliano na Somaliland ya kutumia moja ya bandari zake. Huku Somalia ikiyataja makubaliano hayo kama kitendo cha uchokozi.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed aliwahi kunukuliwa siku za nyuma akisema kuwa matumizi ya bahari ni suala muhimu kwa nchi yake.

Mkataba huo pia umekosolewa vikali na Serikali ya Shirikisho ya Somalia.

Somaliland ilijitenga na Somalia zaidi ya miaka 30 iliyopita, lakini haitambuliki kimataifa.

**BBC**

**Hata hivyo, mzozo wa kidiplomasia kati ya Somalia na Ethiopia umeibuka baada ya Ethiopia kutia saini makubaliano na Somaliland ya kutumia moja ya bandari zake. Huku Somalia ikiyataja makubaliano hayo kama kitendo cha uchokozi.**

# Utawala Hamas wasambaratishwa Gaza Kaskazini

**TEL AVIV, Israel**

MSEMAJI wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, amesema uongozi wa Hamas umesambaratishwa Gaza Kaskazini na kwamba wanamgambo hao kwa sasa wanaendesha shughuli zao katika eneo hilo bila ya makamanda.

Aliyabainisha hayo jana, akiongeza kuwa Israel iliwaua karibu wanamgambo 8,000 kaskazini mwa Gaza, licha ya kwamba idadi hiyo haijathibitishwa moja kwa moja.

Pia ilielezwa kuwa vikosi vya ulinzi vya Israel (IDF) sasa vinalenga kuisambaratisha Hamas Kusini na katikati mwa Gaza.

Naye Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alinukuliwa akisema kuwa Israel itaendeleza kampeni yake ya kuiondoa Hamas, kuwarudisha mateka na kuhakikisha kuwa Gaza haitakuwa tishio tena kwa Israel.

"Tunapaswa kuweka kila kitu pembeni ... hadi ushindi kamili upatikane," alisema Netanyahu.

Wakati huo huo, Hezbollah ilirusha makumi ya roketi kaskazini mwa Israel Jumamosi, katika kile ilichokiita jibu la awali kwa mauaji ya ofisa wa ngazi ya juu wa Hamas huko Beirut wiki iliyopita.

**BBC**

# TWFA MOROGORO WACHAGUANA, MWANDISHI IPP AIBUKA KIDEDEA

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

CHAMA cha Soka la Wanawake (TWFA) Mkoa wa Morogoro, kimefanikiwa kupata viongozi wapya watakaokiongoza kwa kipindi kingine cha miaka minne kwa kumchagua aliyekuwa Katibu wao, Beatrice Selemani kuwa mwenyekiti huku pia mwandishi wa IPP, Idda Mushi, akiibuka kidedea katika nafasi ya uwakilishi wa mkutano mkuu.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika jana katika Shule ya Sekondari ya Bungo mjini Morogoro, msimamizi wa uchaguzi huo, Deo Achimpota, alisema Beatrice ambaye alikuwa hana mpinzani katika nafasi hiyo, alishinda kwa kupata kura zote 12 za ndio kutoka kwa wajumbe 12 wawakilishi wa wilaya sita za Mkoa wa Morogoro huku wilaya moja ya Malinyi ikishindwa kupeleka wawakilishi.

Mwandishi wa Habari wa IPP, Idda, pia alitangazwa kuibuka kidedea kwa kupata kura zote 12 na kumbwaga Jack Meena, aliyekuwa akitetea nafasi yake ya uwakilishi wa mkutano mkuu.

Mwingine aliyechaguliwa ni Flora ambaye hakuwapo kutokana na dharura, lakini alishinda nafasi ya ujumbe wa mkoa huku nafasi mbili za katibu na mjumbe mwingine wa mkoa zikikosa wagombea na uamuzi wa kuwapata wakuziba nafasi ukiachwa kwa viongozi wapya waliochaguliwa.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Mwenyekiti wa TWFA Mkoa wa Morogoro, Beatrice, alisema soka la wanawake mkoani humo linakabiliwa na changamoto ya elimu ndogo ya utambuzi kwa jamii kuhusiana na umuhimu wake na kufanya mabinti wengi kukumbwa na vikwazo katika kujitokeza kushiriki mchezo huo.

Hata hivyo, akataja hatua ambayo uongozi huo unaenda kutekeleza kuwa ni kuifikia jamii kwa kuwapa elimu kwa uwazi ya namna mchezo wa soka ulivyogeuka kuwa fursa adimu kwa watoto wakike katika soko la ajira.

"Katika kipindi hiki cha miaka minne, tuliyopewa kuongoza, moja ya eneo tukalofanyia kazi ni kuinua soka la wanawake, ninatambua bado jamii inakabiliwa na uelewa mdogo wa utabuzi wa soka la wanawake, kwa kuwa bado wengi wao wanaotaka kushiriki wanakumbana na vikwazo katika jamii na familia," alisema Beatrice.

Aidha, aliwapongeza viongozi na wadau wa soka la wanawake waliojitokeza katika uchaguzi huo ambao aliwania nafasi hiyo pasipo kuwa na mpinzani na wapigakura walioshiriki kumpitisha kwa kura zote ndio. Kwa upande wake Idda Mushi, alisema watahakikisha wanaenda kuweka nguvu ya pamoja na viongozi wa ngazi za wilaya katika kuanzisha Ligi za Wanawake maeneo ya vijijini ili kuibua vipaji vipya na kuongeza hamasa kwa watoto wa kike kujitokeza zaidi kushiriki soka.

„Mikakati mingine ni pamoja na kutafuta wafadhili watakaofadhili mashindano mbalimbali yatakayoanzishwa pamoja na vifaa vya michezo," alisema.

Alisema kwa miaka minne ya uongozi wao, wanatarajia kuanzia vijijini kuibua vipaji vya watoto wa kike katika mchezo wa soka ili kuvipa nafasi ya kuonekana huku wakitazamia kufanya kazi karibu na klabu za soka za wanawake zilizopo kwa sasa mkoani humo.

Naye Mwenyekiti Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), Paschal Kihanga, mbali na kuwapongeza viongozi waliochaguliwa, aliwasihi kufanya kazi kwa ushirikiano, kuepuka misuaguano inayoweza kukwamisha mikakati ambayo wamepanga kwenda kuitekeleza.

"Binafsi nawapongezeni kwa kuchaguliwa kuongoza gurudmu hili, viongozi waliokuwapo walikuwa hawana malumbano, shirikianeni kwa umoja, ikitokea kuna jambo halipo sawa, kutaneni mpate ufumbuzi kwa pamoja, hakikisheni hamruhusu kelele zenye kuvuruga mikakati mtakayokwenda kutekeleza," alisema Kihanga.

## Pelembeka, Banja waita mashabiki pambano 'Mtata Mtatuzi' Zanzibar

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Hemed Pelembeka wa Dar es Salaam, ametamba vikali atamchapa mpinzani wake, Mussa Banja wa Zanzibar katika pambano lao la ‚Mtata Mtatuzi' litakalofanyika Januari 27, mwaka huu visiwani Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe wakati akiendelea kujiimarisha, alisema hana wasiwasi na pambano hilo kwani ana uwezo mzuri.

„Ninaendelea kuimarisha mwili wangu kuhakikisha ninawapa burudani mashabiki wangu, ninaomba wajitokeze kwa wingi siku ya pambano," alisema Pelembeka.

Bondia huyo alisema kulingana na mazoezi anayoyafanya hana wasi wasi, hivyo kumtaka mpinzani wake huyo asubiri kichapo.

Kwa upande wa Banja, alisema anamsubiri kwa hamu mpinzani wake na kudai hamhofii licha ya baadhi ya watu kubeza mabondia wa Zanzibar.

„Ninamsubiri kwa hamu mpinzani wangu, nataka nimwoneshe kuwa Zanzibar kuna mabondia wenye vipaji kuliko walivyo mabondia wa Tanzania Bara, alisema Banja.

Aliongeza kuwa atahakikisha anamkalisha mapema kabla ya raundi kumalizika ili azibe midomo ya watu wanaowabeza mabondia wa Zanzibar.



**MAANDALIZI...**



Wachezaji wa Simba, Shomari Kapombe, Saido Ntibazonkiza, Luis Miquison na Moses Phiri, wakiwa mazoezini kujiandaa na mchezo wao wa Kombe la Mapinduzi hatua ya robo fainali dhidi ya Jamhuri, utakaopigwa leo katika Uwanja wa New Amaan Sports Complex, mjini Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

# Stand United yaomba radhi kupigwa sita

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokea kichapo cha kufungulia mwaka cha mabao 6-1 dhidi ya TMA, Klabu ya Stand United imeomba radhi kwa mashabiki wake kutokana na matokeo hayo mabaya.

Juzi, ikiwa nyumbani Uwanja wa Mwadui Complex, Stand United ilikumbana na kipigo hicho kitakatifu kilichowakera mashabiki wake, ambao walianza kuondoka kabla ya mechi kumalizika.

Ulikuwa ni mchezaji wa kwanza wa mzunguko wa pili Ligi ya Championship, kusaka timu mbili zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara moja kwa moja msimu ujao, moja ikisubiri mechi za mchujo.

„Tunaomba radhi kwa matokeo. Mechi imemalizika kwa idadi kubwa ya mabao na hii ni kwa mara ya kwanza kwenye historia ya timu yetu.

„Uongozi pamoja na wachezaji tunaomba radhi kwa wanachama na mashabiki wa ‚Chama la Wana', kila mmoja kwa nafasi yake alipashwa kufanya zaidi ya haya tuliyofanya hii leo (juzi).

„Bado tunayo nafasi ya kufanya vizuri, tuna mechi 14 zingine mbele yetu, hii imeisha tunaendelea kupambana," iliandikwa taarifa hiyo baada ya mechi hiyo kumalizika.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa kocha Mwaka Mwalwisi, baada ya kuichukua TMA, ikiibuka na ushindi wa mabao ya Abdulaziz Shahame aliyepiga ‚hat-trick', Francis Ng'amba aliyepiga mawili na Ally Shomari bao moja, huku la kufutia machozi la Stand United likifungwa na Dennis Richard kwa mkwaju wa penalti.

Katika mechi zingine, Pan African ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Copco kwenye Uwanja wa Mabatini, Pwani saa nane mchana, saa 10:00 jioni Green Warriors ikalazimishwa suluhu dhidi ya Mbeya City, na katika Uwanja wa Ushirika, Moshi, Polisi Tanzania iliichapa Mbeya Kwanza bao 1-0.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HENERSON KURUDI ENGLAND
KIUNGO wa kati wa England, Jordan Henderson, mwenye umri wa miaka 33, anataka kurudi Ligi Kuu England kutoka timu ya Saudi Arabia, Al Ettifaq na atazingatia kwa uzito mapendekezo yoyote yatakayowasilishwa kwa klabu hiyo mwezi huu. **(Mail)**

### GALLAGHER ATAKA KUBAKI
CONOR Gallagher anatarajiwa kubaki Chelsea mwezi huu licha ya Tottenham Hotspur kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. **(Mirror)**

### TIERNEY KURUDISHWA ARSENAL
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta huenda akamrudisha mlinzi wa Scotland, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 26, kutoka uhamisho wa mkopo pale Real Sociedad katika dirisha hili la uhamisho la Januari. **(Football Insider)**

### OLISE AWANIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inataka kumsajili kiungo wa kati wa Crystal Palace, Michael Olise, mwenye umri wa miaka 22, na huenda ikamtumia mlinzi wa England Aaron Wan-Bissaka, mwenye umri wa miaka 26, kama sehemu ya makubaliano hayo. **(Star)**

### INGS ALENGWA WOLVES
KLABU ya Wolves inaangalia uhamisho wa mkopo katika dirisha la uhamisho Januari hii wakati Danny Ings mwenye umri wa miaka 31, wa West Ham akiwa miongoni mwa walengwa wakuu. **(Telegraph)**

### MEJBRI AMULIKWA EVERTON
KLABU ya Everton inajaribu kuipiku Sevilla katika kumwania kwa mkopo mchezaji wa kiungo cha kati wa Tunisia mwenye umri wa miaka 20, Hannibal Mejbri kutoka Manchester United. **(Fabrizio Romano)**

### BERGWIJN ATAJWA WEST HAM
WEST Ham inafikiria kumwania winga wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Steven Bergwijn, 26. **(Sun)**

### KIMMICH ANYATIWA CITY
KLABU ya Manchester City ipo tayari kusubiri mpaka majira ya joto kabla ya kujaribu kumsajili mchezaji wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 28, katika ombi la kutaka kumsajili kwa gharama iliyopungua. **(Mirror)**

### BRUYNE AWINDWA SAUDIA
KEVIN de Bruyne wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, anaendelea kusakwa sana na klabu kuu za Ligi ya Saudi Arabia katika dirisha la uhamisho kwenye majira ya joto. **(Football Insider)**

### DJALO AKARIBIA JUVE
JUVENTUS inajaribu kufikia makubaliano binafsi na beki wa kati wa timu ya Lille raia wa Ureno, Tiago Djalo, mwenye umri wa miaka 23 ambaye anasakwa na Inter Milan. **(Fabrizio Romano)**

### BAYERN YAMFUATA ARAUJO
KLABU ya Bayern Munich haijakata tamaa kumwania mlinzi wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uruguay, Ronald Araujo licha ya kwamba ombi la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, huenda lisikubaliwe katika dirisha la uhamisho la Januari. **(Sky Sports Germany)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# WERNER ATUA TOTTENHAM

**Ametaka kwenda kwa mkopo, kwani anahitaji kucheza michuano ya Euro 2024...**

**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur imefikia makubaliano ya kumsajili Timo Werner kwa mkopo kutoka RB Leipzig na chaguo la kumnunua, kwa mujibu wa ESPN.

Spurs wameingia sokoni kutafuta mshambuliaji mwingine pamoja na kuongeza nguvu kwenye beki wa kati, huku mazungumzo yakiendelea na Genoa kuhusu beki Radu Dragusin.

Nia yao kwa Werner iliibuka Jumamosi asubuhi na David Ornstein wa gazeti la The Athletic, ameripoti kuwa makubaliano kamili yapo kwa Tottenham kumchukua Mjerumani huyo kwa mkopo wa awali kwa msimu uliosalia wa 2023/24.

Mkataba huo una kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa thamani ya kati pauni milioni 13 na 17.

Mapema wiki hii, 90min iliripotiwa kwamba, Werner alikuwa anatazamwa na Manchester United katika harakati zao za kutafuta mshambuliaji na 'Mashetani Wekundu' hao walikuwa wamefanya mawasiliano na Leipzig, lakini sasa atasafiri hadi London kufanyiwa uchunguzi wa afya na kukamilisha uhamisho wa kwenda Spurs.

Werner anaweza kucheza mechi yake ya kwanza kwa Tottenham dhidi ya Man United wakati timu hizo mbili zitakapokutana Old Trafford kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumapili ijayo.

Leipzig ilithibitisha hivi majuzi kwamba Werner alikuwa kwenye mazungumzo na klabu ambayo haikutajwa na kocha Marco Rose alifichua kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alitaka muda wa kucheza zaidi kabla ya kuanza kwa michuano ya Euro 2024 itakayofanyika nchini kwao, Ujerumani.

„Anataka kwenda kwa mkopo, tunamtakia kila la kheri. Anahitaji kucheza kwani anataka kwenda Euro 2024," alisema Rose akiiambia Sky Sports.

Werner anatazamiwa kurejea Ligi Kuu England baada ya misimu miwili mchanganyiko akiwa na Chelsea.

Alifunga mara 23 katika mechi 89 alizoichezea 'The Blues' na kuwasaidia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mara nyingi alikosolewa kwa kutokuwa makini mbele ya goli.

Tottenham walimtafuta Werner kwa mara ya kwanza mwaka wa 2015 alipokuwa kijana akitokea Stuttgart, lakini hawakuweza kukubaliana naye na badala yake wakamsajili Son Heung-min kutoka Bayer Leverkusen.

Son bado yuko Spurs hadi leo na aliteuliwa kuwa nahodha wa klabu kwa msimu wa 2023/24.

# HENDERSON ATAMANI KURUDI KUCHEZA EPL

**RIYADH, Saudi Aarabia**

JORDAN Henderson anafikiria kuondoka Saudi Arabia miezi sita pekee baada ya kujiunga na Al Ettifaq kutoka Liverpool kwa mujibu wa ripoti ya Daily Mail.

Kiungo huyo aliondoka Liverpool Julai mwaka huu baada ya miaka 12 pale Anfield, ili kusajiliwa na Al Ettifaq inayonolewa na Kocha Steven Gerrard, akiungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa timu hiyo na England.

Hata hivyo, gazeti la Daily Mail limeripoti Henderson 'anatamani kurejea Ligi Kuu England', huku akiwa tayari kukatwa mshahara mkubwa na uwezekano wa kulipa bili ya ushuru ya karibu pauni milioni saba ili kupata uhamisho wa dirisha hili la uhamisho.

Mshahara wake wa pauni 700,000 kwa wiki hautozwi ushuru ikiwa atakaa kwa angalau miaka miwili.

Henderson inasemekana kapata ugumu wa kuzoea maisha ya Saudi Arabia, huku hali ya joto ya juu ni sababu zinazochangia kutokuwa na furaha.

Al Ettifaq pia wametatizika kuteka umati mkubwa wa watu msimu huu, ikiwa ni wastani wa mahudhurio ya watu 7,800 pekee licha ya kucheza katika uwanja unaoingiza watu 35,000.

Gerrard naye amekalia kuti kavu baada ya Al Ettifaq kuwa nafasi ya nane kwenye msimamo wa Saudi Pro League, huku msaidizi wake, Ian Foster - ambaye alisaidia kumshawishi Henderson kuhamia Mashariki ya Kati - aliondoka kuchukua kazi ya Kocha wa Plymouth Argyle wiki hii.

Ingawa Henderson angependa kujiunga na kikosi cha Ligi Kuu England, ripoti hiyo inaongeza kuwa klabu nyingi za EPL zitakuwa na shida kupata fedha zinazohitajika kukidhi matakwa yake ya mshahara hata kama atapunguza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amecheza mechi 19 akiwa na Al Ettifaq msimu huu na kusajili asisti tano.




# Tierney aigomea Arsenal

**LONDON, England**

KIERAN Tierney amekataa kusitisha muda wake wa mkopo na Real Sociedad ili kurejea Arsenal mwezi huu.

Beki huyo wa kushoto wa Scotland alijiunga na Sociedad kwa mkataba wa msimu mzima wakati wa majira ya joto baada ya kupoteza nafasi yake Arsenal kwa Oleksandr Zinchenko, ambaye jeraha lake la mguu hivi karibuni limewafanya 'Washikabunduki' hao kukosa mlinzi wa kushoto katika kikosi cha kwanza.

Kocha Mikel Arteta amemtumia beki wa kati Jakub Kiwior kama mlinzi wa kushoto, pamoja na beki wa kulia Takehiro Tomiyasu, lakini baadhi ya mashabiki wameitaka Arsenal kumrudisha Tierney ili kuimarisha kikosi chao kwa muda uliosalia wa msimu.

Tierney alipoulizwa na Noticias de Gipuzkoa kuhusu uvumi wa kutakiwa kurudi Arsenal, alithibitisha na kusema hatarejea Arsenal mapema.

"Watu kadhaa wameniuliza kuhusu hili, lakini jibu langu ni hapana. Hakika ninasalia hapa," alisema Tierney.

"Mashabiki wa Arsenal ni wazuri, walinipa sapoti kubwa. Kwa miaka minne niliyokuwapo pale, nitaendelea kuwashukuru mashabiki."

Huku Zinchenko akiwa ameumia na Tomiyasu sasa anaondoka klabuni hapo kuelekea Kombe la Asia, Arsenal hawana beki wa kushoto na Arteta alikiri wakati wa mkutano na waandishi wa habari Ijumaa kwamba kuna uwezekano wa kusajili beki mpya.

"Tuko wazi kwa soko la uhamisho, lakini msisitizo ni katika kutumia vema kile tulichonacho," alisema Arteta akiviambia vyombo vya habari.

"Tutashirikiana na klabu kuona kama tuna uwezekano wowote au chaguo zuri. Kwanza kabisa tutazingatia wachezaji ambao tunao."

Hata hivyo, Arteta alithibitisha kwamba kusajili beki mpya pia kuna uwezekano.

Mkopo wa Tierney na Sociedad haujumuishi chaguo la uhamisho wa kudumu na hivyo Mskotishi huyo atarejea Arsenal majira ya joto, wakati atakuwa amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake.

# Man United kumwongeza mkataba Varane

**MANCHESTER, England**

RAPHAEL Varane anaweza kupewa nafasi ya kubakia Manchester United kwa masharti yaliyopunguzwa anapokaribia mwisho wa mkataba wake wa sasa, 90min imeripoti.

'Mashetani Wekundu' hao awali walikataa kuanzisha kipengele chao cha nyongeza cha miezi 12 katika mkataba wa Varane, ambao unatarajiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto, huku kukiwa na wasiwasi juu ya gharama ya mkataba wake wa sasa.

Man United wanataka kuketi na Varane kujadili mkataba mpya ambao ukikubaliwa utamfanya mlinzi huyo wa Ufaransa kulipwa mshahara mdogo.

Vyanzo vimeiambia 90min kwamba Varane anaweza kufikiria chaguo kama hilo, baada ya kusema wazi kwamba anatarajia kumaliza kazi yake katika moja ya timu tatu ambazo amewakilisha katika maisha yake ya mazuri kisoka.

Varane aliibuka kama nyota wa ujana huko Lens kabla ya kuimarisha kiwango chake kama mmoja wa mabeki bora wa kizazi chake akiwa na Real Madrid.

Madrid kwa sasa hawafikirii kumnunua Varane, huku Kocha Carlo Ancelotti hivi majuzi akithibitisha kuwa hawatamsajili beki mpya wa kati mwezi huu.

Licha ya nia ya Varane kukwepa kujiunga na timu mpya, 90min inaelewa kuwa maofisa wa Saudi Arabia wako tayari kumpa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ofa msimu wa majira ya joto na wana matumaini kuhusu nafasi yao ya kumshawishi Varane kuhama.

Hadi sasa Varane hajatoa mapendekezo yoyote kwamba atapokea ofa kutoka Saudi Arabia, lakini Mfuko wa Uwekezaji wa Umma, ambao unamiliki vigogo wanne wa nchi hiyo, wanaamini katika uwezo wao wa kuibua maslahi ya mchezaji yeyote.

Kocha Erik ten Hag alithibitisha wakati wa mkutano na waandishi wa habari Alhamisi kwamba United wameanzisha kipengele cha kuongeza mkataba katika mikataba ya Victor Lindelof, Aaron Wan-Bissaka na Hannibal Mejbri, akiongeza kuwa mazungumzo bado yapo kwa Varane na mshambuliaji Anthony Martial, ambaye mkataba wake pia unamalizika msimu huu wa majira ya joto.

HABARI MICHEZO

# KATWILA ATAKA WA4 WAPYA MTIBWA, KAPAMA ATAJWA

Na Saada Akida

ZIKIWA zimebaki siku nane kuanzia leo kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa Januari 16, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, ameweka wazi juu ya nafasi anazotaka kuongeza nguvu ikieleza kuwa kipa, beki, kiungo na mshambuliaji.

Wakati Katwila akitaja nafasi hizo kuna taarifa kuwa kipa aliyetemwa na Coastal Union, Justine Ndikumana na kiungo wa Simba, Nassor Kapamba anayedaiwa huenda akatolewa kwa mkopo, tayari uongozi wa Mtibwa Sugar umeingia mawindoni kusaka saini zao.

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema katika mapendekezo yake ametaka kuongezewa watu wanne katika nafasi hizo ili kuboresha kikosi cha timu kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema kulingana na mapendekezo yake, endapo atawapata wachezaji hao anaamini watafanya kazi nzuri na kuitoa timu hiyo katika nafasi ya chini waliopo kwa sasa katika msimamo wa ligi hiyo.

Mtibwa Sugar ambayo imebakiza mchezo mmoja kabla ya kukamilisha mechi za mzunguko wa kwanza, inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi nane baada kushinda mechi mbili tu na sare mbili huku ikiongoza kwa kuruhusu mabao mengi zaidi (29) hadi sasa.

Kuhusu kuwasajili wachezaji hao wawili, Nipashe lilipomuuliza Katwila alisema: "Siwezi kuzungumzia juu ya wachezaji hao kwa sababu bado hawajafika kambini, nilikabidhi mapendekezo kwa mtendaji mkuu wa timu kufanyia kazi. Kama tutapata huduma zao itakuwa vizuri kwa sababu watakuja kusaidia timu.

"Unajua suala la mkopo hadi mchezaji akubali kama atatolewa na kujiunga kwetu, ninaimani kubwa uongozi unafuata mapendekezo ambayo nimewapa ikiwamo kuboresha baadhi ya nafasi ninazohitaji kuimarisha timu yetu."

FA CUP...



Beki wa kulia wa Aston Villa, Matty Cash, akishangilia na kupongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yake bao katika dakika za mwisho dhidi ya Middlesbrough, na kuiwezesha kutinga raundi ya nne ya Kombe la FA England kwa ushindi wa 1-0 juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Pan African yatakiwa kumaliza tofauti zao

Na Saada Akida

MWENYEKITI wa Pan African SC, Adam Kirumbi, amewataka wanachama wa timu hiyo kuweka kando tofauti zao na kuwa kitu kimoja ili kuweza kurejesha heshima ya klabu hiyo pamoja na kunusuru jengo lao ambalo kesi ipo mahakamani.

Jengo hilo kiwanja namba 9, kitalu Na. 34, lililopo eneo la Kariakoo, Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam, lipo katika mgogoro kati ya mmiliki na mwekezaji ambaye aliingia makubaliano na uongozi uliopita.

Akizungumza na Nipashe jana, katika kikao cha dharura cha wanachama wa timu hiyo, Kirumbi alisema kumekuwa na mpasuko na mgawanyiko baina ya baadhi ya wanachama na uongozi uliomaliza muda wake.

Alisema mnamo Oktoba 8, mwaka jana baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Pan Afrika, alitoa ahadi ya kuhakikisha anamaliza mpasuko huo na kurudisha umoja wa klabu hiyo jambo ambalo wamelitekeleza.

"Mimi na baadhi ya wajumbe wa bodi ya utendaji tuliitisha kikao cha pamoja na baadhi ya wanachama walikuwa na uhusiano mzuri na uongozi uliomaliza muda, tuliwapa nafasi wanachama kunieleza na kutoa dukuduku zao na kuweka jambo hilo sawa.

„Lakini pia kuna malalamiko makubwa ya wanachama kwa mkataba mbovu wa ubia ulioingiwa na uongozi uliopita, ilidaiwa jengo letu kuuzwa, tunapaswa kurudi kuhakikisha Pan Afrika inaendeshwa kwa kufuata katiba ili kutokomeza hayo yote," alisema Kirumbi.



## Gamondi awaandalia mfumo wapaki basi

INATOKA UK. 24

na kumalizika AFCON hakutokuwa na muda tena," alisema kocha huyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema katika aina mpya ya mazoezi ya Gamondi alikuwa anadili na viungo, mawinga na washambuliaji tu.

„Gamondi katika mfumo huu au staili hii mpya ya uchezaji hana kazi na mabeki, anadili na viungo, mawinga na washambuliaji tu, zinapigwa pasi, mashuti.

„Yamefungwa mabao mengi sana siku ya kwanza ya mfumo huu mazoezini, zaidi ya mabao 17, zinapigwa pasi, halafu anawekewa mtu nje ya 18, Shekhan amefunga mabao kama sita peke yake kwa mashuti ya mbali, Maxi Nzengeli naye ametandika mabao ya kutosha, Skudu (Mahlatse Makudubela) naye kafunga, naona huko mbele tutakuwa na staili nyingi za kufunga mabao na si mpaka tuingie ndani ya eneo la hatari," alisema Kamwe.

Yanga inashika nafasi ya pili katika Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 30, lakini inakamata nafasi ya pili ya Kundi D, Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa na pointi tano sawa na kinara Al Ahly ya Misri ambayo ina kiporo cha mechi moja.

## Kocha Azam: Kwa Sarr, Simba imelamba dume

INATOKA UK. 24

alisema ujio wa kiungo huyo utaenda kutibu matatizo yote ya kiulinzi ya timu yao.

Alisema miaka ya hivi karibuni wamekuwa wakikosa namba sita asilia, hivyo baada ya kutua kiungo huyo, wanaimani tatizo limetatulika, tangu alivyoondoka James Kotei, Gerson Fraga na Teddeo Lwanga, hawajapata kiungo asilia wa ukabaji.

"Tumepambana kupata saini ya kiungo Sarr, ni mchezaji tuliyemkosa katika timu yetu kwa muda mrefu, tumekuwa na wachezaji bora, lakini hatukuwa na namba sita asilia. Sasa kati patakuwa na Sarr, Sadio Kanoute, Mzamiru Yassin na Abdallah Hamis, tutakuwa na safu bora sana ya kiungo," alisema Ahmed.

Michezo
Jumatatu Januari 8, 2024
Nipashe

Werner atua Tottenham UKURASA 21



# GAMONDI AWAANDALIA MFUMO WAPAKI BASI

## ●●● Nzengeli, Skudu wampatia majibu mapema, asema sasa anataka hata nje ya...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameanza kutengeneza mfumo mpya wa uchezaji ili kuwafanya wachezaji wake waweze kufunga mabao mengi, hasa kwa timu ambazo ‚zinapaki basi' (zinakaa nyuma ya mpira) mwanzo mwisho.

Kuelekea katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya APR ya Rwanda iliyochezwa jana usiku kwenye Uwanja wa New Amaan Sports Complex, Zanzibar, Gamondi aliamua kuwafundisha vijana wake jinsi ya kujipanga na kuachia mashuti makali ya mbali huku akiwataka si lazima wafike hadi langoni.

Akizungumza kutoka Zanzibar, kocha huyo alisema hajafundisha mfumo huo kwa ajili ya mechi ya robo fainali dhidi ya APR tu, bali hata mechi zingine zinazofuata za Kombe la Mapinduzi na hasa Ligi Kuu pamoja na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema mazoezi yanayofanyika visiwani humo si kwa ajili ya michuano hiyo pekee, bali hata michuano mingine ijayo.

„Tuna Kombe la Mapinduzi, lakini tuma michuano mingine mingi, mazoezi haya ni kwa ajili ya maandalizi yote kwani huu ndiyo muda mzuri wa kujiandaa tukitoka hapa

INAENDELEA UK. 23



Maxi Nzengeli

# Kocha Azam: Kwa Sarr, Simba imelamba dume

**Na Saada Akida**

HUKU akipelekwa Zanzibar haraka jana kujiunga na wachezaji wenzake wanaoshiriki Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssoupha Dabo, amechungulia ‚jembe jipya' lililosajiliwa Simba, Babacar Sarr na kuweka wazi huo ni usajili bora uliofanywa na uongozi wa ‚Wekundu wa Msimbazi' hao katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

Simba juzi walimtambulisha rasmi kiungo huyo raia wa Senegal na jana kumpeleka visiwani Zanzibar kujiunga na wachezaji wenzake wanaoshiriki Kombe la Mapinduzi.

Dabo ambaye naye ni raia wa Senegal, kabla ya kuja Tanzania aliwahi kufanya kazi na Sarr wakati anaichezea Klabu ya Teungueth ya Ligi Kuu nchini humo pamoja na Gibril Silla na Pape Ousamane Sakho.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema usajili walioufanya Simba kwa kuinasa saini ya kiungo mkabaji, Sarr ni moja ya sajili bora kwa sababu ya kipaji kikubwa alichonacho kitakwenda kusaidia sana timu hiyo.

Alisema anafahamu uwezo na ubora wa nyota huyo, hivyo anaimani usajili huo utaongeza kitu kwenye nafasi ya kiungo na kuisaidia sana Simba akishirikiana vema na wachezaji wenzake ndani ya timu hiyo.

„Sarr ni kijana wangu nilikuwa naye Teungueth miaka miwili iliyopita, ni kiungo mzuri na mchezaji bora anayejua kupambana, hapa Simba wamepata mtu na atawasaidia sana katika timu yao.

„Huu ni usajili bora kwao na nimefurahia kumuona ni sehemu ya soka la Tanzania, namkaribisha na nitamsaidia kuzoea mazingira si kwenye timu bali nchini kwa sababu nina baadhi ya taarifa ya baadhi ya maeneo," alisema Dabo.

Aliongeza kabla ya kutua nchini amekuwa akiwasiliana naye kwa kipindi kirefu tangu alipokuwa nchini Tunisia, hivyo anaamini hii itakuwa nafasi yake ya kuonana naye tena.

Wakati huo Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally,

INAENDELEA UK. 23



Babacar Sarr

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA ... UARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >